


# Wilaya ya Shule ya Hyde Park Central

*2025 - 2026*

# Kanuni za Maadili Mema

# Barua Kutoka kwa Msimamizi Mkuu

Jamii Pendwa ya Wilaya ya Shule ya Hyde Park Central,

Karibu katika mwaka wa shule wa 2025-2026! Tunapofungua mwaka mwingine uliojaa fursa na matumaini, tunaahidi zaidi kukuza mazingira ya mafunzo yanayofaa na yasiyo na ubaguzi ambapo kila mwanafunzi na mfanyakazi wanaweza kunawiri. Jukumu letu la pamoja ni kuhakikisha kuna nafasi salama, zenye heshima na za kushirikisha zinazokuza ufanisi wa kielimu, ukuaji wa mtu binafsi na ukuzaji wa tabia thabiti.

Tumapoendelea kusonga mbele, tunaongozwa na Maono na Dhamira ya wilaya yetu:

**Dhamira:** *Tunawawezesha wanafunzi wote kuwa wanajamii fanisi katika jamii yetu inayobadilika mara kwa mara.*
**Maono:** *HPCSD ni jamii bunifu ya mafunzo kwa wote.*

Msingi wa kufanikisha dhamira na maono haya ni kazi tunayofanya kila siku ili kuhakikisha kuwa shule zetu zinabaki kuwa mahali ambapo kila mwanafunzi anahisi anathaminiwa, anaisidika na yuko salama. Ahadi hii inajitokeza kwenye Mwongozo wetu wa Kanuni za Maadili Mema, ambao unatumika kama msaada na mwongozo kwa wanafunzi, familia na wafanyakazi.

Kanuni za Maadili Mema zinatokana na kanuni za msingi zifuatazo:

- *Kuwasaidia wanafunzi kuwa raia wawajibikaji na wenye heshima kwa kuwafunza kutofautisha mema na mabaya.*
- *Kuhimiza kufanya maamuzi ya busara na kuwajibika kibinafsi.*
- *Kuwawajibisha wanajamii wote wa shule yetu kwa vitendo na maneno yao.*
- *Kuwa mfano wa tabia nzuri tunazotaka kukuza katika wanafunzi wetu.*

Mwongozo wa Kanuni za Maadili Mema unawakilisha juhudi za pamoja za wasimamizi, waalimu, wanafunzi, wazazi/walezi, wanajamii na wafanyakazi wanaokuja pamoja ili kukagua kwa makini na kuboresha sera zinazokuza mazingira salama na yenye mpangilio ya mafunzo. Utaratibu huu wa kina unahakikisha kuwa matarajio yaliyoelezwa yanaeleweka, hayabadiliki na yanalingana na maadili yetu ya pamoja. Kama kawaida, Mwongozo utaendelea kukaguliwa kila mwaka ili ulingane na mahitaji yanayobadilika ya jamii ya shule yetu.

Katika kufuata dhamira yetu ya kielimu, nidhamu katika shule yetu inachukuliwa kama fursa ya mafunzo na ukuaji. Tunaendelea kujitolea kutumia hatua za urekebishaji ili kurekebisha madhara, kujenga upya imani na kuimarisha mahusiano. Lengo letu si tu kurekebisha tabia, lakini pia ni kuwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wa kudumu maishani katika kujidhibiti, kuwa na huruma na kufanya maamuzi kwa uwajibikaji.

Tuna furaha kushirikiana nawe tunapofanya kazi pamoja kuwaandaa wanafunzi wetu kuwa raia wawajibikaji, wadadisi wa mambo, wanafunzi wa kujiamini, wawasilianaji bora na wabunifu wepesi. Asante kwa kuendelea kutusaidia kufanya HPCSD kuwa mahali salama, wazi na panapovutia kwa wote. Ninamtakia kila mtu mwaka wa shule wenye furaha na mafanikio!

Kwa Fahari ya Hyde Park,




## Wanakamati

Melissa Lawson
Dkt. Pedro Roman
Margaret Qatani
Michael Tibbetts
Joanna Murphy
Joanna Mikula
Megan D'Alessandro
Eric Shaw
Jennifer Malizia
Nancy Hulton
Jessica Cole
Colleen Colburn
Roman Pemberton
Ray Labulis
Colton Palmatier
Guiseppe Doran
Juan Rivera
Jovanni Rivera
Meaghan Doolittle
Lisa Foster

# Yaliyomo


Barua Kutoka kwa Msimamizi Mkuu ........ 2
Wanakamati ........ 2
Utangulizi ........ 4
Kwa nini tuna kanuni za maadili mema? ........ 5
Tabia Tano Zinazotarajiwa ........ 6
Haki na Wajibu wa Wanafunzi Wetu ........ 8
Washirika Muhimu ........ 9
- Wazazi/Walezi/Watunzaji ........ 9
- Wafanyakazi ........ 9

Wageni Wanaotembelea Shule Zetu ........ 12
Tabia ya Umma Shuleni ........ 12
- Tabia Inayokatazwa ........ 12
- Hatua za kuchukuliwa ........ 13
- Utekelezaji wa Sheria ........ 13

Kuchukua Hatua na Uzuiaji wa Uchokozi na Usumbufu ........ 14
- Ufafanuzi ........ 14
- Uzuiaji ........ 15
- Msaada ........ 15
- Huduma kwa Wanafunzi Wanaohofia Usalama Wao ........ 15
- Kuripoti na Kuchunguzwa kwa Tukio ........ 15
- Hatua za Adhabu/Urekebishaji ........ 16
- Kutolipiza Kisasi ........ 16
- Mafunzo ........ 16
- Usambazaji, Ufuatiliaji na Ukaguzi ........ 16

Kuripoti Ukiukaji ........ 17
- Usiri ........ 17

Tabia ya Mwanafunzi Inayokatazwa ........ 18
Kanuni za Mavazi ya Mwanafunzi ........ 20
Adhabu, Tarartibu na Maelekezo ........ 21
- Hatua za kuchukuliwa ........ 22
- Taratibu ........ 23
- Adhabu ya Wanafunzi wenye Ulemavu ........ 28
- Mpango Mwingine wa Mafunzo ........ 32
- Upekuzi na Kumhoji Mwanafunzi ........ 33
- Adhabu ya Kuchapwa ........ 34

Usambazaji na Ukaguzi ........ 35
Kiambatisho cha A: Kamusi ya Maneno ........ 36
Kiambatisho cha B: Fomu ya Mwanafunzi ya Kuwasilisha Malalamiko ya Uchokozi na Kusumbuliwa ........ 37


*Sera zetu zote zinapatikana kwenye tovuti yetu: https://go.boarddocs.com/ny/hpcsd/Board.nsf/Public

# Utangulizi

Bodi ya Elimu imejitolea kuwezesha mazingira ya shule ambayo ni salama na yenye mpangilio ambapo wanafunzi wanaweza kupokea na wafanyakazi wa wilaya wanaweza kutoa huduma bora za elimu bila kuvurugwa au usumbufu. Wilaya ya shule imejitolea:

- kuhakikisha kila mwanafunzi ni mwenye afya, yuko salama, anashirikishwa, anasaidiwa na kupewa changamoto;
- kuwasaidia wanafunzi kukuza nidhamu binafsi na ukuaji wa kijamii na kihisia; na
- kuwaelekeza wanafunzi katika uboreshaji na urekebishaji wa tabia zisiofaa ambazo hazikubaliki na si salama.

Tabia ya uwajibikaji inatarajiwa kutoka kwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine wa wilaya, mzazi/wazazi na wageni wengine, kwa kuwa ni muhimu katika ufanikishaji wa lengo hili.



Ili hili litendeke, kila mtu katika jamii ya shule lazima aonyeshe na awaheshimu wengine.

Kwa kutambua kuwa watoto wote hukosea na kuwa hii ni sehemu ya ukuaji, shule lazima ziawasaidie wanafunzi wote kujifunza kukua kutokana na makosa yao. Sera za kuadhibu za shule zinapaswa kuwasaidia wanafunzi na walimu na kuhakikisha kuwa hadhi na heshimu ya kila mtu inadumishwa.

Ushirikishaji wa wanafunzi pia ni muhimu katika kuwezesha mazingira na utamaduni mzuri wa shule unaokuza vizuri mafanikio ya kielimu ya wanafunzi na ukuaji wa kijamii/kihisia. Kuwapa wanafunzi fursa nyingi za kushiriki katika shughuli nyingi za kijamii huku pia wakikuza uhusiano na watu wazima wanaojali na wenye msaada hupunguza tabia mbaya. Mifano inaweza kujumuisha: kuwapa wanafunzi fursa zenye maana za kubadilishana mawazo na habari na kushiriki katika miradi ya jumla ya shule; ukuzaji wa ujuzi wa uongozi wa mwanafunzi; utambuaji wa mara kwa mara wa mafanikio ya mwanafunzi katika sehemu mbalimbali za kielimu na nje ya elimu ya darasani; kutumia majibu ya urekebishaji; na kukuza mifumo ya jumla ya shule ya kuhimiza tabia nzuri.

Wilaya ina matarajio yaliyowekwa kuhusu tabia inayofaa ukiwa shuleni na katika shughuli za shule. Matarajio haya yanatokana na kanuni za ustaarabu, kuheshimiana, uraia, tabia, uvumilivu, uaminifu na uadilifu.

Watu wote wakiwa shuleni lazima waonyeshe tabia salama. Inapohitajika na wilaya wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa kuambukiza, hii inaweza kujumuisha kukaa umbali unaofaa na wengine na kuvaa maski au vifaa vingine vya kujilinda.

Bodi inatambua haja ya kufafanua kwa uwazi matarajio haya ya tabia inayokubalika ukiwa shuleni, kutambua hatua zinazoweza kuchukuliwa kuhusu tabia isiyokubalika zilizopimwa na zinazofaa kulingana na umri, na kuhakikisha kuwa adhabu, panapohitajika, inatolewa kwa wakati unaofaa na kwa haki, kwa kukumbuka kuwa lengo si kuadhibu, lakini ni kuwafunza wanafunzi kuwa kuna matokeo kwa vitendo na maamuzi yao. Kwa hivyo, Bodi imetunga kanuni hizi za maadili mema (“kanuni”), zinazotokana na sheria na kanuni za elimu na sera za Bodi.

Isipokuwa ifafanuliwe vinginevyo, kanuni hizi zinatumika kwa wanafunzi wote, wafanyakazi wa shule, mzazi/wazazi na wageni wengine wakiwa shuleni au wanapohudhuria shughuli ya shule.

# Kwa nini tuna kanuni za maadili mema?

1. Wanafunzi wanahitaji kusaidiwa na kushirikishwa shuleni ili kukuza tabia thabiti na mwenendo unaofaa. Ni muhimu pia wanafunzi waweze kuwajibika kulingana na umri kwa tabia zao binafsi.

Ushirikishaji wa wanafunzi hukuzwa wanafunzi wanapopewa fursa nyingi za kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii wakiwa wanashirikiana na watu wazima wanaojali na wenye msaada. Hii husaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaweza:

- kutambua na kudhibiti hisia;
- kukuza hali ya kuwajali wengine;
- kujenga mahusiano mazuri;
- kufanya maamuzi ya busara; na
- kushughulikia hali zenye changamoto ipasavyo na kimaadili.

2. Maagizo yanayofaa na ya kushirikisha na misaada mizuri ya kitabia ni misingi ya mazingira mazuri ya shule. Walimu, wasimamizi na wafanyakazi wengine wote wa shule wanatarajiwa kuweka viwango vya juu vya ufanisi wa wanafunzi, kujenga mahusiano mazuri na wanafunzi, pamoja na kufunza na kuwa mfano wa tabia zinazofaa ili kufaulu. Kuwa mfano wa tabia nzuri yenye heshima ni muhimu hasa wakati kuchukua hatua za adhabu.

3. Watu wazima wote, walimu wakuu, wasimamizi, wafanyakazi wa shule, mzazi/wazazi na jamii kwa ujumla wana jukumu la kuwasaidia wanafunzi kuwa raia wema na kuishi maisha yenye maana kwa kuwa mfano wa tabia zinazotarajiwa na kukuza tabia hizo ndani ya wanafunzi.

4. Mwenendo unaofaa na tabia thabiti hujitokeza katika mazingira ya kijamii, yenye heshima, mazuri na yenye kujali. Sera na desturi za kuadhibu na kumsaidia mwanafunzi zitatekelezwa kwa njia ya kujali na kwa usawa, yenye heshima na kulingana na kuaminiana kati ya wasimamizi, wafanyakazi, wanafunzi na familia na zinazowawajibisha watu wote, zinazorekebisha na zinazolenga suluhu. Hii itawasaidia wanafunzi:

- kujifunza kutokana na makosa yao;
- kuelewa kwa nini tabia yao haikubaliki;
- kukubali madhara waliyosababisha au athari mbaya za vitendo vyao;
- kuelewa kile ambacho wangefanya tofauti;
- kuwajibika kwa vitendo vyao;
- kujifunza mikakati ya kujenga mahusiano mazuri ya kijamii na ujuzi wa kutumia baadaye; na
- kuelewa kuwa matokeo na/au hatua zaidi zitachukuliwa ikiwa tabia zao zisizokubalika zitaendelea.

5. Wilaya itaendelea kufuatilia matokeo kwa juhudi za kutambua mikakati ya uboreshaji.



# Tabia Tano Zinazotarajiwa kwa Jamii ya Shule ya Hyde Park

Utekelezaji wa tabia za kawaida zinazotarajiwa katika wilaya yetu ya shule ni mkakati wa msingi wa kukuza uthabiti, usawa na mazingira mazuri ya mafunzo kwa wanafunzi wote. Mfumo wa pamoja wa tabia unasababisha uelewaji na utiifu kati ya wanafunzi, wafanyakazi na familia, na kuhakikisha kuwa kila mwanajamii wa shule anaelewa kinachotarajiwa na jinsi ya kukuza tabia inayofaa.

Ili kuendeleza mbinu hii ya pamoja, wilaya imetunga tabia tano za kawaida zinazotarajiwa, kila moja ikiwa na vifafanuzi vinavyoeleweka vya kuwaelekeza wanafunzi na wafanyakazi. Matarajio haya matano yanatumika kama msingi wa utamaduni wa wilaya ambapo wanafunzi hawawajibishwi tu lakini pia wanasaidiwa kuwa washirika wenye mchango katika jamii za shule yao.

**Jiheshimu, Waheshimu Wengine na Uheshimu Mazingira**

- Jivunie
- Heshimu thamani ya kila mtu
- Sherehekea utofauti
- Kuza umoja
- Wezesha mazingira ya mafunzo yenye usalama wa kihisia na ushirikiano
- Wasikilize wengine
- Kubali maoni tofauti
- Zungumza na utende kwa ukarimu na kujali
- Tumia lugha ya adabu
- Tumia sauti inayofaa mahali ulipo
- Tunza na uthamini mali ya shule na mali ya wengine

**Onyesha Uadilifu**

- Kuwa mwaminifu
- Fanya jambo sahili
- Kuwa rafiki mwema
- Kuwa mtu wa kutegemewa
- Kubali maoni
- Kuwa na mtazamo wa ukuaji
- Fanya kazi yako binafsi/fikiria mwenyewe
- Kubali makosa yako
- Shiriki katika hatua za urekebishaji panapohitajika
- Usiogope kushindwa
- Omba usaidizi unapohitajika
- Shirikiana vizuri na wengine
- Tambua wengine (tambua na urejelee vyanzo)
- Fanya maamuzi mazuri

**Wajibika**

- Fuata kanuni na matarajio
- Fanya bidii
- Fuata maelekezo
- Tunza wakati
- Kuja shuleni isipokuwa uwe mgonjwa
- Kuwepo
- Fanya kazi na majukumu yako vizuri zaidi kadri uwezavyo
- Omba usaidizi unapohitajika
- Kuwa tayari kujifunza na kushiriki kikamilifu
- Fikiria kivyako
- Shiriki katika shughuli (vilabu, muziki, michezo, uongozi wa wanafunzi, nk.)

**Kuwa Mkakamavu**

- Wajibika kwa vitendo vyako
- Onyesha bidii
- Kuwa na msimamo
- Kuwa mwepesi kurekebika
- Vumilia
- Fanikisha malengo yako
- Kuwa mwepesi kubadilika
- Tumia huduma za usaidizi zinapotolewa au zinapohitajika
- Jaribu ukishindwa mara ya kwanza

**Tenda kwa Usalama**

- Heshimu nafasi ya wengine
- Tenda kwa njia salama
- Fuata kanuni
- Zingatia zaidi afya yako
- Tenda kwa uangalifu
- Timiza ahadi
- Jifunze tabia ya kutafakari
- Tumia zana ipasavyo, ikijumuisha teknolojia
- Kuwa mmoja wa kuhakikisha mazingira salama
- Safisha kabla hujaondoka



Ili kukuza mazingira ya mafunzo ambayo ni salama, yenye heshima na mazuri, tabia zinazotarajiwa hufafanuliwa kwa uwazi na kutekelezwa kwa uthabiti katika maeneo yote ya shule.

| Eneo | Kuwa na Heshima | Onyesha Uadilifu | Wajibika | Kuwa Mkakamavu | Tenda kwa Usalama |
|---|---|---|---|---|---|
| *Darasani* | Tumia maneno ya upole na utunze vifaa na nafasi | Fanya kazi kwa uaminifu na ufuate kanuni za darasa | Kuwa tayari na uombe usaidizi panapohitajika | Endelea kujaribu wakati mambo ni magumu | Baki kwenye kiti chako na utumie vifaa ipasavyo |
| *Njia za Ukumbi* | Tembea polepole na uwaruhusu wengine wapite | Nenda moja kwa moja mahali unapopaswa kuwa | Usichafue njia ya ukumbi na uzingatie jukumu lako | Kuwa mtulivu wakati wa vipindi vya mabadiliko | Tembea ukiwa umeangalia mbele; usirushe mikono na miguu |
| *Kafeteria* | Kuwa na tabia nzuri za mezani na uwape wengine nafasi | Fuata kanuni na usafishe kabla hujaondoka | Kula chakula chako na ufuate maelekezo ya mtu mzima | Subiri kwa uvumilivu kwenye laini na udhibiti hisia zako | Baki kwenye kiti; tumia chakula na vyombo ipasavyo |
| *Uwanjani* | Shirikiana, cheza kwa zamu na utumie maneno ya upole | Cheza kwa haki na ufuate kanuni | Cheza kwa haki na ufuate kanuni | Jaribu michezo mipya na ujikwamue kutokana na kushindwa | Tumia vifaa vizuri na uripoti tabia isiyo salama |
| *Vyumba vya kujisaidia* | Subiri mwingine atoke na usichafue mahali hapo | Tumia vyumba vya kujisaidia inavyohitajika tu | Rudi darasani haraka na utunze wakati | Fanya maamuzi mazuri bila kusimamiwa moja kwa moja | Tembea, tumia vifaa vizuri na uoshe mikono |
| *Kufika na Kuondoka* | Wasalimu wengine ipasavyo na ufuate maelekezo | Kuwa mahali unapopaswa kuwa | Fika kwa wakti na uwe tayari | Vumilia hali za kucheleweshwa au mabadiliko | Tembea kwa upole na ukae katika maeneo yaliyotengwa |
| *Basi* | Wazungumzie wanafunzi an dereva kwa upole; usichafue basi | Fuata kanuni za basi hata bila kukumbushwa | Fika kwa wakati, kaa kwenye kiti chako na ulinde vitu vyako | Kubali kwa upole mabadiliko ya viti na hali za kucheleweshwa | Baki kwenye kiti chako na usirushe mikono na miguu na vitu |

# Haki na Wajibu wa Wanafunzi Wetu

**A. Haki za Mwanafunzi**

Wilaya imejitolea kulinda haki za wanafunzi wote kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo na sera ya wilaya. Kuongezea, ili kuwezesha mazingira ya shule ambayo ni salama, yenye afya, yenye mpangilio na yenye msaada, wanafunzi wote katika wilaya wana haki ya:

1. Kushiriki katika shughuli zote za wilaya kwa usawa bila kujali asili ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), uzito, rangi, imani, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, jinsia (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi au ulemavu.
2. Kuheshimiwa kama mtu binafsi na kutendewa kwa haki na kwa heshima na wanafunzi wengine na wafanyakazi wa shule.
3. Kutoa maoni yao, iwe kwa matamshi au kwa maandishi, mradi wafanye hivyo kwa njia ya heshima.
4. Kuelezea upande wao wa matukio husika kwa wafanyakazi wa shule waliopwa idhini ya kuchukua hatua.
5. Kupata na kusoma hati ya sera, sheria na kanuni za shule, na panapohitajika, kufafanuliwa kanuni hizo na mfanyakazi wa shule.
    a. Kuelezewa kwa uwazi matarajio kuhusu:
    b. Malengo ya kozi, mahitaji na viwango vya jimbo;
    c. Mfumo na taratibu za kupewa gredi;
    d. Mahitaji ya kazi za shuleni na mwisho wa kuziwasilisha; na
    e. Kanuni za shuleni na darasani na tabia zinazotarajiwa.

**B. Majukumu ya Mwanafunzi**



Wanafunzi wote katika wilaya wana jukumu la:

1. Kuchangia katika udumishaji wa mazingira ya shule ambayo ni salama, yenye msaada na yenye mpangilio yanayofaa kwa mafunzo na kuwaheshimu watu wengine na mali.
2. Kusaidia kufanya shule kuwa jamii ambayo haina vurugu, vitisho, uchokozi, usumbufu na ubaguzi.
3. Kufahamu na kufuata sera, sheria na kanuni za wilaya zinazoshughulikia tabia ya mwanafunzi.
4. Kwenda shuleni kila siku isipokuwa awe ameomba ruhusa rasmi na kuwa darasani kwa wakati na kuwa tayari kujifunza.
5. Kufanya bidii kadri awezavyo katika shughuli zote za kielimu na za nje ya elimu ya darasani na kujitahidi kufikia kiwango chake cha juu zaidi cha mafanikio iwezekanavyo.
6. Kufuata mwelekeo anaopewa na walimu, wasimamizi na wafanyakazi wengine wa shule kwa njia nzuri na ya heshima.
7. Kutumia sauti ya upole na lugha ya mwili inayofaa, kusikiliza wakati wengine wanakuzungumzia.
8. Kusema ukweli anapozungumza na maafisa wa shule kuhusu makosa ya uvunjaji wa Kanuni za Maadili Mema.
9. Kuheshimu nafsi ya mtu binafsi.
10. Kujitahidi kukuza ujuzi wa kudhibiti hisia na vitendo vyake na kusuluhisha mgogoro na wengine.
11. Kuuliza maswali wakati haelewi.
12. Kuomba usaidizi wa kutatua matatizo.
13. Kuvaa ipasavyo shuleni na katika shughuli za shule.
14. Kukubali kuwajibika kwa vitendo vyao.
15. Kujichukua kama wawakilishi wa wilaya wanaposhiriki au wanapohudhuria matukio ya shule ya nje ya elimu ya darasani na kuonyesha viwango vya juu zaidi vya tabia, adabu na uanaspoti.

# Washirika Muhimu

Washirika wote wa jamii yetu ya mafunzo - ikijumuisha wanafunzi, wafanyakazi, wazazi na watoa huduma wanaoshirikishwa lazima wawajibike katika kukuza tabia inayoimarisha ufanisi wa kielimu na kijamii. Tabia yenye adabu, heshima na uwajibikaji huwezesha mazingira mazuri katika jamii ya mafunzo.

Majukumu hayo ni pamoja na, lakini si tu yafuatayo:

**A. Wazazi/Walezi/Watunzaji**

Kanuni za Maadili Mema ni mwongozo wa kuelewa tabia za kibinafsi, kijamii na kielimu zinazotarajiwa kutoka kwa mtoto wako akiwa shuleni na katika shughuli za shule. Kanuni hizi pia zinaelekeza jinsi wafanyakazi wa shule watakavyoshirikiana nawe na mtoto wako ili kusaidia kuonyesha tabia nzuri na kufurahia ufanisi wa kielimu.

Ili kufanikisha lengo hili, wazazi wote wanatarjiwa:

1. Kutambua kuwa elimu ya mtoto/watoto wao ni jukumu la pamoja la wazazi na jamii ya shule na kushirikiana na wilaya ili kuboresha fursa za kielimu za mtoto wao.
2. Kuwapeleka watoto wao shuleni wakiwa tayari kushiriki na kujifunza.
3. Kuhakikisha watoto wao wanaenda shuleni kila siku kwa wakati unaofaa.
4. Kuhakikisha wanaomba ruhusa wanapokosa kwenda shuleni.
5. Kuhakikisha watoto wao wamevaa na wametayarishwa kwa njia inayolingana na mwongozo wa kanuni za maadili mema.
6. Kuwasaidia watoto kuelewa kuwa katika jamii huru kanuni zinazofaa zinahitajika ili kudumisha mazingira salama na yenye mpangilio.
7. Kujua kanuni za shule na kuwasaidia watoto wao kuzielewa ili waweze kusaidia kuwezesha mazingira ya shule ambayo ni salama, yenye heshima na yenye msaada.
8. Kuwafunza watoto wao kuwa na hisia ya kupenda elimu na wilaya.
9. Kujenga mahusiano mazuri yenye maana na walimu, wazazi wengine na marafiki wa watoto wao.
10. Kuwaambia maafisa wa shule kuhusu wasiwasi au malalamiko yoyote kwa njia ya heshima na kwa wakati unaofaa.
11. Kuwasaidia watoto wao kukabiliana vizuri na msukumo wa wenzao.
12. Kuwafahamisha maafisa wa shule kuhusu mabadiliko katika hali ya nyumbani yanayoweza kuathiri tabia au utendaji wa mwanafunzi.
13. Kutengeneza mahali pa kusomea na kuhakikisha kazi za shule za kufanyia nyumbani zinafanywa.
14. Kuwa wenye heshima na adabu kwa wafanyakazi, wazazi/walezi wengine na wanafunzi wakiwa shuleni na katika hali zote za ushirikiano na mawasiliano.
15. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

**B. Wafanyakazi**

Kanuni za Maadili Mema ni mwongozo wa kukuza tabia nzuri ya mwanafunzi shuleni. Unakusudiwa kuwasaidia wafanyakazi kuzuia tabia ya mwanafunzi isiyofaa kupitia utumiaji wa mikakati na mifumo inayofaa. Utatoa mwongozo wa kuchukua hatua inayofaa na ipasavyo ikwia wanafunzi hawatatimiza viwango vya tabia vilivyowekwa au wakivunja kanuni na sera za shule. Masuala kuhusu usalama na mazingira ya shule yanapaswa kuripotiwa kwa mwalimu mkuu wa shule ili wafanyakazi waweze kushirikiana pamoja ili kudumisha mazingira ya mafunzo na kazi ambayo ni salama na yenye mpangilio.

Wafanyakazi wote wanatarajiwa kuelewa kuwa wanafunzi wanaweza kuja shuleni wakiwa wamepitia hali ngumu za maisha, ambazo zinaweza kuathiri tabia yao shuleni (k.m., hasira, milipuko ya hasira, kutojali, kujiumiza).

1. Walimu: Ili kufanikisha lengo hili, walimu wote katika wilaya wanatarajiwa:
    a. Kudumisha mazingira ya kuheshimiana na kuheshimu wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au jinsia, ambavyo vitaimarisha hali ya mwanafunzi kujithamini na kukuza imani ya kusoma.
    b. Kuwa tayari kufunza.
    c. Kuonyesha hali ya kupenda kufunza na kuwajali wanafunzi na mafanikio ya mwanafunzi.
    d. Kujua sera na kanuni za shule na kuzitekeleza kwa njia ya haki, kwa wakati unaofaa na kwa uthabiti.
    e. Kudumisha usiri kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo.

f. Kuwaeleza wanafunzi na wazazi:
  i. Malengo na mahitaji ya kozi
  ii. Tataribu za kusahihisha/kupeana gredi
  iii. Mwisho wa kuwasilisha kazi ya shuleni
  iv. Matarajio kutoka kwa wanafunzi
  v. Tabia ya darasani na mpango wa kuchukua hatua.

g. Kuwasiliana mara kwa mara na wanafunzi, wazazi na walimu wengine kuhusu ukuaji na mafanikio.

h. Kushiriki katika juhudi za shuleni za kutoa usimamizi wa kutosha katika maeneo yote ya shule, kulingana na Sheria ya Taylor (Taylor Law).

i. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.

j. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote shuleni au darasani.

k. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

2. Washauri wa Shuleni:

a. Kudumisha mazingira ya kuheshimiana na kuheshimu wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au jinsia.

b. Kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na msukumo wa wenzao na matatizo ya kibinafsi, kijamii na kihisia yanayoibuka.

c. Kuandaa mikutano ya mwalimu/mwanafunzi/mshauri na mikutano ya mzazi/ mwalimu/ mwanafunzi/ mshauri, panapohitajika, kama njia ya kusuluhisha matatizo.

d. Kukagua na wanafunzi mara kwa mara maendeleo yao ya kielimu na mipango ya taaluma.

e. Kudumisha usiri kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo.

f. Kutoa maelezo ya kuwasaidia wanafunzi kupanga taaluma zai.

g. Kuwatia moyo wanafunzi kufaidika kutokana na mtaala na mipango ya nje ya elimu ya darasani.

h. Kuwafahamisha wanafunzi na familia kuhusu huduma zinazopatikana katika jamii zinazoweza kutimiza mahitaji yao.

i. Kushiriki katika juhudi za shuleni za kutoa usimamizi wa kutosha katika maeneo yote ya shule.

j. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.

k. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote.

l. Kuhimiza utumiaji wa mbinu inayotambua changamoto ya kiakili katika kushughulikia tabia ya mwanafunzi kwa kusaidia katika maendeleo ya kitaalamu, kuwezesha mazingira salama ya kazi, kujenga mahusiano ya kuaminiana na wanafunzi, kuwaruhusu wanafunzi kufanya maamuzi yao wenyewe na kuwapa uhuru, na kuhimiza ukuzaji wa ujuzi na ustadi wa mwanafunzi.

m. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

3. Wafanyakazi Wengine wa Shuleni:

a. Kudumisha mazingira ya kuheshimiana na kuheshimu wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au jinsia.

b. Kudumisha usiri kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo.

c. Kufahamu kanuni za maadili mema.

d. Kuwasaidia watoto kuelewa matarajio ya wilaya ya kudumisha mazingira salama yenye mpangilio.

e. Kushiriki katika juhudi za shuleni za kutoa usimamizi wa kutosha katika maeneo yote ya shule.

f. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.

g. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote.

h. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

4. Walimu Wakuu/Wasimamizi:

a. Kukuza mazingira ya shuleni ambayo ni salama, yenye mpangilio na ya kuchochea, kuwezesha mafunzo na kujifunza kikamilifu kwa wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au jinsia.

b. Kuhakikisha kuwa wanafunzi na wafanyakazi wana fursa ya kuwasiliana na mwalimu mkuu/wasimamizi.

c. Kudumisha usiri kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo. Kulingana na sheria ya FERPA, shule au wilaya ya shule inaweza kutoa maelezo yanayomtambulisha mtu (Personally Identifiable Information, PII) kutoka kwenye rekodi za elimu bila idhini kwa washirika wa timu ya ukadiriaji wa hatari ambao si wafanyakazi wa shule au wilaya ya shule ikiwa wanatimiza masharti ya kutambuliwa kama "maafisa wa shule" wenye "maslahi halali ya kielimu".

d. Kukagua mipango yote ya mafunzo mara kwa mara ili kuhakikisha ujumuishaji wa elimu ya ustaarabu katika mtaala.
e. Kusaidia katika ukuzaji na kushiriki kwa mwanafunzi katika shughuli zinazofaa za nje ya elimu ya darasani.
f. Kusaidia katika utunzi wa kanuni za maadili mema, wanapohitajika. Kusambaza kanuni za maadili mema na sera za kukataza usumbufu.
g. Kuwajibika katika utekelezaji wa kanuni za maadili mema na kuhakikisha kuwa kesi zote zinasuluhishwa haraka iwezekanavyo na kwa haki.
h. Kushiriki katika juhudi za shuleni za kutoa usimamizi wa kutosha katika maeneo yote ya shule.
i. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.
j. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote na wafanyakazi.
k. Kuhimiza utumiaji wa mbinu inayotambua changamoto ya kiakili katika kushughulikia tabia ya mwanafunzi kwa kusaidia katika maendeleo ya kitaalamu, kuwezesha mazingira salama ya kazi, kujenga mahusiano ya kuaminiana na wanafunzi, kuwaruhusu wanafunzi kufanya maamuzi yao wenyewe na kuwapa uhuru, na kuhimiza ukuzaji wa ujuzi na ustadi wa mwanafunzi.
l. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

5. Msimamizi/Wasimamizi wa Sheria ya Heshima (Dignity Act):

Msimamizi/Wasimamizi wa Sheria ya Heshima (Dignity Act Coordinator(s)) ni Waalimu Wakuu wa shule katika shule zao; Manaibu Walimu Wakuu wanaweza kuhudumu kama wawakilishi wa Mwalimu Mkuu wakati Mwalimu Mkuu hayupo na Naibu Msimamizi wa Huduma za Wanafunzi ndiye Msimamizi wa Sheria ya Heshima katika kiwango cha Wilaya. Wana majukumu yafuatayo:

a. Kukuza mazingira ya shuleni ambayo ni salama, yenye mpangilio na ya kuchochea, kuwezesha mafunzo na kujifunza kikamilifu kwa wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi, (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia) au jinsia.
b. Kusimamia na kupanga kazi ya kamati za uzuiaji wa uchokozi katika kiwango cha shule na katika wilaya nzima.
c. Kutambua nyenzo za mtaala zinazosaidia kujumuisha ustaarabu katika mafunzo ya darasani na usimamizi wa darasa; na kutoa mwongozo kwa wafanyakazi wa jinsi ya kufikia na kutekeleza nyenzo hizo.
d. Kushiriki katika juhudi za shuleni za kutoa usimamizi wa kutosha katika maeneo yote ya shule.
e. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.
f. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote na wafanyakazi.
g. Kuhimiza utumiaji wa mbinu inayotambua changamoto ya kiakili katika kushughulikia tabia ya mwanafunzi kwa kusaidia katika maendeleo ya kitaalamu na kuajiri wafanyakazi wanaofaa.
h. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

7. Bodi ya Elimu:

a. Kukuza mazingira ya shuleni ambayo ni salama, yenye mpangilio na ya kuchochea, kuwezesha mafunzo na kujifunza kikamilifu kwa wanafunzi wote bila kujali asili yao ya kweli au inayodhaniwa, (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi au jinsia.
b. Kudumisha usiri kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo.
c. Kubuni na kupendekeza bajeti inayotoa mipango na shughuli zinazosaidia katika ufanikishaji wa malengo ya kanuni za maadili mema.
d. Kushirikiana na mwanafunzi, mwalimu, msimamizi na mashirika ya wazazi, wafanyakazi wa usalama wa shule na wafanyakazi wengine wa shule kutunga kanuni za maadili mema zinazoeleza kwa uwazi tabia zinazotarajiwa kutoka kwa wanafunzi, wafanyakazi wa wilaya na wageni wakiwa shuleni na katika shughuli za shule.
e. Kupitisha na kukagua angalau kila mwaka kanuni za maadili mema za wilaya ili kutathmini ufanisi wa kanuni hizo na uhaki na uthabiti wa utekelezaji wake.
f. Kuwa kielelezo kwa kuendesha mikutano ya Bodi kwa njia ya kitaalamu, yenye heshima na adabu.
g. Kushughulikia masuala ya usumbufu au hali yoyote inayotishia afya ya kihisia au kimwili au usalama wa mwanafunzi yeyote, mfanyakazi wa shule au mtu yeyote aliye shuleni kisheria au katika shughuli ya shule.
h. Kushughulikia mapendeleo ya kibinafsi yanayoweza kuzuia usawa katika kuwashughulikia wanafunzi wote na wafanyakazi.
i. Bodi inapaswa kuhimiza utumiaji wa mbinu inayotambua changamoto ya kiakili katika kushughulikia tabia ya mwanafunzi kwa kusaidia katika maendeleo ya kitaalamu, kuwezesha mazingira salama ya shule, kuhimiza kujenga mahusiano ya kuaminiana na wanafunzi, kuwaruhusu wanafunzi kufanya maamuzi yao wenyewe na kuwapa uhuru, na kuhimiza ukuzaji wa ujuzi na ustadi wa mwanafunzi.
j. Kuwa tayari kushiriki kikamilifu katika usuluhishaji wa migogoro kupitia utaratibu wa urekebishaji.

# Wageni Wanaotembelea Shule Zetu

Bodi inatambua kuwa ufanisi wa mpango wa shule unategemea, kwa sehemu, usaidizi kutoka kwa jamii kwa ujumla. Bodi ingependa kuwezesha mazingira mazuri ambapo wanajamii wana fursa ya kuona bidii na mafanikio ya wanafunzi, walimu na wafanyakazi wengine. Kwa kuwa shule ni mahali pa kazi na mafunzo, hata hivyo, mipaka fulani lazima iwekwe kwa wageni hao. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake anawajibika kwa watu wote wanaoingia shuleni na uwanjani. Kwa sababu hizi, yafuatayo yanatarajiwa kutoka wageni shuleni:

1. Mtu yeyote ambaye si mfanyakazi wa kawaida au mwanafunzi wa shule atachukuliwa kuwa mgeni.
2. Wageni wote wanaokuja shuleni lazima waingie kupitia lango moja lililotengwa na kuripoti kwenye kituo cha mapokezi au kwenye Ofisi ya Mwalimu Mkuu baada ya kufika shuleni. Huko watatoa kitambulisho cha picha, watatia saini kwenye rejesta ya wageni na watapewa beji ya kumtambulisha mgeni, ambayo lazima waivae wakati wote wakiwa shuleni au kwenye uwanja wa shule. Mgeni lazima arudishe beji hiyo kwenye lango kuu la kuingia kabla ya kuondoka shuleni.
3. Wageni wanaohudhuria shughuli za shule ambazo ni za wazi kwa watu wote baada ya saa za kawaida za shule, kama vile mikutano ya shirika la wazazi na walimu au mikutano ya raia hawahitajiki kuripoti kuingia.
4. Mzazi/wazazi au raia ambao wangependa kuona darasa au shughuli ya shule wakati shule inaendelea, lazima wapange ziara hizo mapema na mwalimu/walimu wa darasa na Mwalimu Mkuu wa Shule.
5. Walimu wanatarajiwa kufunza na hawataweza kuchukua muda wa darasa kujadili masuala ya kibinafsi na wageni.
6. Mtu yeyote atakayeingia shuleni bila idhini ataripotiwa kwa Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake. Watu watakaoingia shuleni bila idhini wataombwa waondoke. Polisi wanaweza kuitwa ikiwa hali italazimu.
7. Wageni wote wanatarajiwa kutimiza matarajio ya tabia za raia zilizo katika kanuni hizi za maadili mema wakiwa shuleni.

# Tabia ya Umma Shuleni

Kwa makusudui ya sehemu hii ya kanuni, neno “umma” linamaanisha watu wote wakiwa shuleni au wanapohudhuria shughuli ya shule ikijumuisha wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa wilaya.

Tabia zinazotarajiwa kutoka kwa raia walio shuleni na katika shughuli za shule hazikusudiwi kuzuia uhuru wa kuzungumza au kufanya mkutano wa amani, lakini zinakusudiwa kuwezesha mazingira mazuri ya mafunzo na kudumisha mpangilio na kuzuia uingiliaji wa haki za wengine.

Watu wote walio shuleni au katika shughuli ya shule lazima wajiendeshe kwa njia salama, yenye heshima na mpangilio. Kuongezea, watu wote walio shuleni au wanaohudhuria shughuli ya shule wanatarajiwa kuvalia mavazi yanayofaa kwa kusudi lililowaleta shuleni.

A. **Tabia Inayokatazwa** - Hakuna mtu, iwe peke yake au na wengine, anayeweza:
    1. Kumwumiza mtu yeyote au kutishia kufanya hivyo, au kuhatarisha usalama wake binafsi au wa wengine.
    2. Kuharibu kimakusudi mali ya wilaya ya shule au mali binafsi ya mwalimu, msimamizi, mfanyakazi mwingine wa wilaya au mtu mwingine aliye shuleni kisheria, ikijumuisha grafiti au kuchoma kwa moto.
    3. Kuvuruga mpangilio wa madarasa, mipango ya shule au shughuli nyingine za shule.
    4. Kusambaza au kuvaa vitu shuleni au katika shughuli za shule ambavyo vina lugha chafu, vinahimiza kitendo cha kinyume cha sheria, vinaonekana kuwa vya kukashifu, vinaingilia haki za wengine au vinavuruga mpango wa shule.
    5. Kutishia, kusumbua au kubagua mtu yeyote kwa msingi wa asili yake ya kweli au inayodhaniwa (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo) imani, rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, jinsia au mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia).
    6. Kuingia katika eneo lolote la shule bila idhini au kubaki kwenye jengo au kituo chochote baada ya saa za kawaida za kufungwa.

7. Kuzuia uhuru wa kutembea wa mtu yeyote mahali popote ambapo kanuni hizi zinatumika.
8. Kuvunja sheria za trafiki, kanuni za uegeshaji au vizuizi vingine kuhusu magari.
9. Kumiliki, kutumia, kuuza, kutoa, kutengeneza, kusambaza au kubadilishana vinywaji vya pombe, vitu vinavyodhibitiwa au vilivyopigwa marufuku kisheria au namna zozote za vitu vilivyotengenezwa kutokana na kemikali (iwe vimebainishwa kuwa vimepigwa marufuku kisheria au la au vimetiwa lebo kuwa vinaweza kutumiwa na binadamu), au kulewa kutokana na mojawapo ya vitu hivyo akiwa shuleni au katika shughuli ya shule.
10. Kumiliki au kutumia silaha shuleni au katika shughuli ya shule, isipokuwa kwa maafisa wa utekelezaji wa sheria au isipokuwa kama ilivyoidhinishwa kwa njia maalum na wilaya ya shule.
11. Kutangatanga shuleni.
12. Kucheza kamari shuleni au katika shughuli za shule.
13. Kukataa kufuata mpangilio wowote unaofaa wa maafisa wa wilaya ya shule wanaotambulika wanaotekeleza majukumu yao.
14. Kuwachochea wengine kimakusudi kutenda vitendo vyovyote vinavyokatazwa na kanuni hizi.
15. Kuvunja sheria yoyote ya kitaifa au ya jimbo, amri ya eneo au sera ya Bodi akiwa shuleni au akiwa katika shughuli ya shule.
16. Kuvuta sigara, biri, bomba, sigara ya kielektroniki (yaani, vape), au kutumia tumbaku ya kutafunwa au isiyotoa moshi, au kuvuta moshi/ mvuke/kula bangi au bangi iliyosindikwa (ikijumuisha bidhaa za bangi) au kuvuta katani ya bangi (isipokuwa kwa matumizi ya kisheria ya matibabu ya bangi kulingana na sheria na kanuni za jimbo).

**B. Hatua za kuchukuliwa** - Watu wanaovunja kanuni hizi watachukuliwa hatua zifuatazo:

1. Wageni: Idhini yao, ikiwa wanayo, ya kubaki katika uwanja wa shule au katika shughuli ya shule itaondolewa na wataamrishwa waondoke shuleni. Wakikataa kuondoka, wataondolewa kwa nguvu.
2. Wanafunzi: Watachukuliwa hatua ya adhabu kulingana na maelezo, kulingana na mahitaji ya utaratibu unaofaa.
3. Wafanyakazi wa shule walioajiriwa: Watachukuliwa hatua ya adhabu kulingana na maelezo, kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha § 3020-a au haki nyingine zozote za kisheria wanazoweza kuwa nazo.
4. Wafanyakazi: Katika huduma iliyoainishwa ya kitengo cha huduma kwa raia inayolindwa na Sheria ya Huduma kwa Raia (Civil Service Law) Kifungu cha § 75. Wataondolewa mara moja na kuchukuliwa hatua ya adhabu kulingana na maelezo, kulingana na Sheria ya Huduma kwa Raia (Civil Service Law) Kifungu cha § 75 au haki nyingine zozote za kisheria wanazoweza kuwa nazo.
5. Wafanyakazi: Isipokuwa walioelezwa katika vifungu vidogo vya 3 na 4. Wataonywa, watakemewa, watasimamishwa kazi kwa muda au kufutwa kulingana na maelezo, kulingana na haki zozote za kisheria wanazoweza kuwa nazo.

**C. Utekelezaji**

Mwalimu Mkuu wa mwakilishi wake anawajibika kwa utekelezaji wa tabia inayohitajika na kanuni hizi.

Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake akimwona mtu akitenda vitendo ambavyo havichangii katika kufanikisha lengo la kufanya shule kuwa jamii ambayo haina vurugu, vitisho, uchokozi, usumbufu na ubaguzi, tabia isiyofaa au vinginevyo tabia zisizoruhusiwa, ambazo kwa busara yake hazisababishi hatari yoyote ya moja kwa moja ya kuumiza watu au kuharibu mali, Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake atamwambia mtu huyo kuwa tabia hiyo hairuhusiwi na kujaribu kumsihi mtu huyo akome. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake atamwonya pia mtu huyo kuhusu hatua atakazochukuliwa asipokoma. Mtu huyo akikataa kukoma kutenda tabia zisizofaa, au ikiwa vitendo vya mtu huyo vinasababisha hatari ya moja kwa moja ya kuumiza watu au kuharibu mali, Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake ataamrisha mtu huyo aondolewe shuleni au katika shughuli ya shule mara moja. Ikihitajika, maafisa wa polisi wataitwa ili wasaidie kumwondoa mtu huyo.



Wilaya itamchukulia mwanafunzi au mfanyakazi yeyote hatua ya adhabu, ipasavyo, kulingana na kifungu cha 'Hatua za Kuchukuliwa" hapa juu. Kuongezea, wilaya ina haki ya kuwasilisha kesi ya kiraia au kihalifu kuhusu mtu yeyote anayevunja kanuni.

# Kuchukua Hatua na Uzuiaji wa Uchokozi na Usumbufu

Bodi ya Elimu imejitolea kuwezesha mazingira ya kielimu na kikazi yanayokuza heshima, hadhi na usawa. Bodi inatambua kuwa ubaguzi, kama vile usumbufu, uaibishaji na uchokozi, ni vikwazo kwa kujifunza na mafanikio ya mwanafunzi. Tabia hizi zinaathiri dhamira ya wilaya ya kuelimisha wanafunzi wake na kuvuruga shughuli za shule. Tabia hiyo haiathiri tu wanafunzi wanaolengwa, lakini pia inaathiri watu wanaoshiriki na kushuhudia vitendo hivyo.

Kwa hivyo, Bodi inakemea na kukataza kabisa namna zote za ubaguzi, kama vile usumbufu, uaibishaji na uchokozi shuleni, kwenye mabasi ya shule na katika shughuli, mipango na matukio yote ya shule. Tabia za ubaguzi, usumbufu, uaibishaji au uchokozi zinazofanyika nje ya shule, kama vile uchokozi wa mtandaoni, ambazo zinasababisha au zinazoweza kutarajiwa kusababisha athari kuu na kubwa kwa mahitaji ya nidhamu inayofaa shuleni au kuingilia haki za wanafunzi wengine zinakatazwa, na zinaweza kusababisha kuchukuliwa hatua za adhabu.

**Ufafanuzi**

1. Uchokozi. Uchokozi, kulingana na Sheria iliyorekebishwa ya Heshima kwa Wanafunzi wote (Dignity for All Students Act), ina maana sawa na usumbufu (angalia hapa chini). Kanuni inayoambatana inatoa mwongozo zaidi kuhusu ufafanuzi na sifa za uchokozi wa kusaidia jamii ya shule kutambua tabia hiyo.

2. Uchokozi wa mtandaoni. Uchokozi wa mtandaoni unafafanuliwa kama usumbufu (angalia hapa chini) kupitia njia yoyote ya mawasiliano ya mtandaoni.

3. Ubaguzi. Ubaguzi ni kitendo cha kunyima haki, manufaa, usawa au uwezo wa kutumia vifaa

vinavyofaa kutumiwa na watu wote, kwa mtu binafsi au kikundi cha watu kwa sababu ya kikundi, tabaka au kitengo ambacho mtu huyo yumo (kama ilivyoelezwa katika kifungu cha Ufafanuzi, chini ya Usumbufu, hapa chini).

4. Uaibishaji. Uaibishaji ni utaratibu wa kukaribishwa, kuapishwa au kufanywa kuwa mshirika unaohusisha usumbufu unaosababisha kuaibishwa mbele ya umma, kuumizwa kimwili au kihisia, kuumizwa mwili au kufanyiwa mzaha mbele ya umma au unaosababisha hali ambapo tukio la kuaibishwa mbele ya umma, kuumizwa kimwili au kihisia, kuumizwa mwili au kufanyiwa mzaha mbele ya umma linaweza kutokea.

5. Usumbufu. Usumbufu umefafanuliwa kwa njia mbalimbali katika sheria na kanuni za kitaifa na za jimbo. Bodi inatambua kuwa fafanuzi hizi ni viwango muhimu, lakini lengo la Bodi ni kuzuia tabia isiyofaa isizidi zaidi ili kukuza mazingira mazuri ya shule na kuzuia kuwajibishwa. Sheria ya Heshima kwa Wanafunzi Wote (Dignity for All Students Act) (Vifungu vya §§10 hadi 18 vya Sheria ya Elimu (Education Law)) inafafanua usumbufu kama usababishaji wa mazingira ya uadui kwa tabia au kwa vitisho, kutishia au kudhulumu, ikijumuisha uchokozi wa mtandaoni, ambao

   (a) una athari au unaweza kusababisha athari ya kuathiri vibaya na kwa kiwango kikubwa elimu, fursa au manufaa au afya ya kiakili, kihisia au kimwili ya mwanafunzi;
   (b) unaotarajiwa kusababisha au unaoweza kutarajiwa kusababisha mwanafunzi kuhofia usalama wake;
   (c) unaotarajiwa kusababisha au unaoweza kutarajiwa kusababisha jeraha la mwili au madhara ya kihisia kwa mwanafunzi; au 5/7/24, 11:00 AM BoardDocs® Pro https://go.boarddocs.com/ny/hpcsd/Board.nsf/Private?open&login# 1/4
   d) unaotokea nje ya shule na kusababisha au unaoweza kutarajiwa kusababisha hatari ya vurugu kubwa ndani ya shule, ambao inatarajiwa kuwa tabia, vitisho, kutishia au dhuluma hiyo inaweza kufika shuleni. Tabia ya usumbufu inaweza kutokana na sifa yoyote, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu:

      - asili ya mtu ya kweli au inayodhaniwa (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu hali na mitindo ya nywele ya kujilinda , ikiwa ni pamoja na, lakini si tu misuko, misokoto na mikunjo),
      - rangi,
      - uzito,
      - taifa la asili,
      - kabila,
      - dini,
      - desturi za kidini,
      - ulemavu,
      - jinsia,
      - mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi,
      - au jinsia (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia).

Kwa makusudi ya ufafanuzi huu, neno "vitisho, kutishia au dhuluma" inajumuisha vitendo vya kimatamshi na vya kiishara.

Wakati mwingine, uchokozi au usumbufu unaweza kusababisha kosa la uvunjaji wa haki za kiraia za mtu. Wilaya inamakinikia sana majukumu yake kulingana na sheria na kulingana na sera ya wilaya kuhusu ulinzi wa haki za kiraia.

Ili kulainisha maneno ya sera na kanuni hii, neno uchokozi litatumika katika hati nzima ili kujumuisha tabia za usumbufu, kutishia, uchokozi wa mtandaoni na uaibishaji.

**Uzuiaji**

Mazingira ya shule yanatoa fursa ya kuwafunza watoto, na yanasisitizia wafanyakazi kuwa ushirikiano na kuheshimiana na wengine ni maadili muhimu ya wilaya. Mpango wa uzuiaji haukusudiwi tu kupunguza matukio ya uchokozi lakini kuwasaidia wanafunzi kujenga mahusiano yenye msaada zaidi na kila mmoja kwa kujumuisha mpango wa uzuiaji wa uchokozi katika mafunzo ya darasani. Wafanyakazi na wanafunzi watahamasishwa, kupitia maendeleo ya kitaalamu na mafunzo katika wilaya nzima, kuhusu dalili za onyo la uchokozi, pamoja na jukumu lao la kuhusika kikamilifu katika uzuiaji wa uchokozi kabla ya vitendo hivyo kutokea.

Nyenzo za mtaala zinazohamasisha na kufahamisha kuhusu ubaguzi au uchokozi na ustaarabu katika mahusiano ya watu wa asili tofauti, uzito, mataifa ya asili, makabila, madini, desturi za kidini, uwezo wa kihisia au kimwili, mielekeo ya kuvutiwa kimapenzi, jinsia au mwonekano au utambulisho wa kijinsia zitajumuishwa katika mpango wa mafunzo kutoka Chekechea hadi gredi ya 12.

Ili kutekeleza mpango huu bodi itatenga Msimamizi wa Sheria ya Heshima (Dignity Act Coordinator, DAC)] wa kuhudhuria mkutano wake wa kishirika wa kila mwaka kwa kila shule katika wilaya. Mmoja wa DAC itatengwa kama msimamizi katika wilaya nzima ambaye majukumu yake yameelezwa kwenye kanuni inayoambatana. Jukumu la kila DAC ni kusimamia na kutekeleza sera hii katika shule ambayo amepewa.

**Msaada**

Msaada wa watu wazima na wapita njia ni hatua muhimu katika kuzuia kuzidi zaidi na kusuluhisha matatizo mapema. Msaada utasisitiza elimu na ukuzaji wa ujuzi.

Msaada wenye ufanisi unaweza kuhusisha hatua za urekebishaji. Hatua za urekebishaji wa tabia ya uchokozi zinajumuisha hatua zinazokusudiwa kurekebisha tabia yenye tatizo, kuzuia tukio lingine la tabia hiyo na kumlinda mlengwa. Hatua za urekebishaji zinaweza kumlenga mtu/watu waliohusika katika tabia ya uchokozi au mbinu za kimazingira zinazolenga shule au wilaya kwa ujumla.

Kuongezea, msaada utalenga usalama wa mlengwa. Wafanyakazi wanatarajiwa, wakiwa na habari kuhusu tukio la uchokozi, waliripoti kulingana na sera hii, kumwelekeza mwanafunzi kwa huduma za usaidizi zilizotengwa, au kuingilia kati kulingana na sera na kanuni hii.

**Huduma kwa Wanafunzi Wanaohofia Usalama Wao**

Bodi inakiri kuwa, licha ya hatua zinazochukuliwa na wafanyakazi wa wilaya, msaada unaweza kuhitaji matumizi ya mbinu maalum iliyopangwa ikiwa mtoto anahofia usalama wake shuleni. Wanafunzi wanaohofia usalama wao shuleni huwa na uwezo mdogo wa kujifunza na kufanikiwa kielimu. Wafanyakazi, wakiwa na habari kuhusu tukio la uchokozi, wanapaswa kutambua ikiwa huduma za msaada zinahitajika ili kusaidia kuhakikisha usalama wa mwanafunzi na kuripoti suala hilo kwa mwalimu mkuu wa shule. Mwalimu mkuu wa shule, wafanyakazi wengine wanaofaa, mwanfunzi na mzazi wa mwanafunzi watashirikiana pamoja ili kutambua na kutekeleza huduma zozote za msaada zinazohitajika.

Wilaya inatambua kuwa kuna haja ya kusawazisha huduma za msaada zinazoimarisha usalama wa mwanafunzi kutokana na uwezekano wa kuaibishwa zaidi kwa mwanafunzi aliyelengwa. Kwa hivyo, kila kesi itashughulikiwa kivyake. Mwanafunzi, mzazi.mlezi na wasimamizi wa shule watashirikiana ili kutambua huduma za usalama zinazolingana vizuri zaidi na mahitaji ya mwanafunzi aliyelengwa. Majadiliano na/au mikutano ya ufuatiliaji itapangwa, inavyohitajika, ili kuhakikisha kuwa wasiwasi wa usalama umeshughulikiwa ipasavyo na kutambua wakati na ikiwa huduma za msaada zinahitaji kubadilishwa au kukomeshwa.

**Kuripoti na Kuchunguzwa kwa Tukio**

Ingawa inaweza kuwa vigumu kujitokeza na kuripoti, wilaya haiwezi kushughulikia ipasavyo tukio la uchokozi ikiwa matukio hayataripotiwa. Wanafunzi ambao wamechokozwa, wazazi ambao watoto wao wamechokozwa au wanafunzi wengine wanaoshuhudia tabia ya uchokozi wanahimizwa na wanatarajiwa kuwasilisha malalamiko kwa matamshi na/au kwa maandishi kwa mfanyakazi yeyote wa shule kulingana na mafunzo na mwongozo uliowekwa. Wafanyakazi wanaoshuhudia au kupata habari kuhusu tukio/matukio ya uchokozi wanahitajika, kulingana na sheria ya Jimbo, kuwasilisha ripoti kwa matamshi kwa mwalimu mkuu wa shule au mwakilishi wake ndani ya siku moja ya shule na kujaza fomu ya kuripoti ya wilaya ndani ya siku mbili za shule. Wafanyakazi ambao hawana uhakika kuhusu utaratibu wa kuripoti wanatarajiwa kuwauliza wasimamizi wao jinsi ya kuripoti. Wafanyakazi wa wilaya wanaweza kuchukuliwa kuwa wameruhusu kitendo cha ubaguzi wa kinyume cha sheria au uchokozi ikiwa hawataripoti tukio waliloshuhudia, hata kama mlengwa ataripoti au hataripoti.

Wakati wote, malalamiko yatarekodiwa, kufuatiliwa na kushughulikiwa kulingana na kanuni na taratibu zinazoambatana na sera hii, au, panaphusika, [0100, Sheria ya Usawa na Kuzuia Ubaguzi (Equal Opportunity and Nondiscrimination), au 0110, Sheria ya Unyanyasaji wa Kijinsia (Sexual Harassment)] na Kanuni za Maadili Mema za wilaya. Mwalimu Mkuu wa Shule au mwakilishi wake atatayarisha ripoti ya kutumwa kwa Msimamizi Mkuu haraka iwezekanavyo kulingana na malalamiko yaliyowasilishwa.

Uchunguzi wenye usawa na wa kina utafanywa na Mwalimu Mkuu wa Shule au mwakilishi wake kulingana na kanuni inayoambatana. Kuongezea, matokeo ya uchunguzi huo yataripotiwa kwa mlengwa na mshtakiwa ilivyoelezwa kwenye kanuni inayoambatana. Ikiwa upande wowote hautakubaliana na matokeo ya uchunguzi, unaweza kukata rufaa kuhusu matokeo hayo kulingana na kanuni zinazoambatana na sera hii. Maukio ya uchokozi yaliyothibitishwa yanayotimiza vigezo vilivyowekwa na jimbo yatajumuishwa kwenye mfumo wa kuripoti wa jimbo panapohusika, kulingana na sheria na kanuni.

**Hatua za Adhabu/Urekebishaji**

Ingawa lengo la sera hii ni kuhusu uzuiaji, vitendo vya uchokozi bado vinaweza kutokea. Katika hali hizi, wakosaji watafahamishwa wazi kuwa vitendo vyao havifai na lazima wabadilishe tabia hiyo. Wakosaji ambao ni wanafunzi watashauriwa shuleni kuhusu kufanya maamuzi mazuri katika mahusiano yao na wengine. Panapofaa, hatua ya adhabu iliyopimwa, iliyosawazishwa na inayolingana na umri itachukuliwa na usimamizi kulingana na Kanuni za Maadili Mema za wilaya, panapohusika. Ikiwa tabia itafikia kiwango cha shughuli ya kihalifu, maafisa wa polisi wataitwa.

Hatua za kuchukuliwa kwa mwanafunzi anayefanya kitendo cha uchokozi zitakuwa za kipekee kulingana na hali maalum na zitatofautiana kwa njia na ukubwa kulingana na hali ya tabia, umri wa ukuaji wa mwanafunzi, na historia ya mwanafunzi ya kuwa na tabia za kutatiza, na lazima zilingane na Kanuni za Maadili Mema za wilaya.

**Kutolipiza Kisasi**

Malalamiko yote na wale wanaoshiriki katika uchunguzi wa malalamiko kulingana na sheria ya jimbo na sera za wilaya, ambao wametenda ipasavyo kwa nia njema, wana haki ya kutolipizwa kisasi cha aina yoyote.

**Mafunzo**

Bodi inatambua kuwa ili kutekeleza mpango fanisi wa uzuiaji wa uchokozi na mpango wa msaada, maendeleo ya kitaalamu yanahitajika. Msimamizi Mkuu, DAC wa wilaya na Timu ya Wilaya ya Maendeleo ya Kitaalamu (District Professional Development Team) watajumuisha mafunzo ya kukuza mpango huu katika maelekezo ya walimu wapya na katika mpango wa kila mwaka wa maendeleo ya kitaalamu, inavyohitajika. Fursa za mafunzo zitatolewa kwa wafanyakazi wote, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu madereva wa basi, kafeteria na wasimamizi wa ukumbi na wafanyakazi wote wanaotangamana na wanafunzi. DAC watafunzwa kulingana na mahitaji ya jimbo na wataendelea na ukuzaji wa taaluma zao ili waweze kuendeleza kwa ufanisi sera na mpango huu.




**Usambazaji, Ufuatiliaji na Ukaguzi**

Sera hii, au muhtasari wa lugha rahisi, utachapishwa kwenye hati za kuandikisha wanafunzi, mwongozo wa mwanafunzi, mzazi na wafanyakazi, na kuchapishwa kwenye tovuti ya wilaya. Fomu ya malalamiko ya uchokozi itapatikana kwenye tovuti ya wilaya. Wilaya itahakikisha kuwa utaratibu wa kuripoti matukio ya uchokozi umefafanuliwa kwa uwazi kwa wanafunzi, wafanyakazi na wazazi kila mwaka.

Kila mwaka, kama sehemu ya ukaguzi wa kila mwaka wa Kanuni za Maadili Mema, sera hii itakaguliwa ili kukadiria ufanisi na utiifu wake wa sheria ya jimbo na ya kitaifa. Ikiwa kuna mabadiliko yanayohitaji kufanywa, marekebisho yatapendekezwa kwa Bodi ili iyakague.

Wilaya itahakikisha kuwa ripoti ya taarifa kuhusu sera hii inatolewa kwa umma kwa njia inayolingana na haki za faragha za wanafunzi chini ya Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (Family Educational Rights and Privacy Act, FERPA).

# Kuripoti Ukiukaji

Kwa sababu lengo la wilaya ni kufanya shule kuwa jamii ambayo haina vurugu, vitisho, uchokozi, usumbufu na ubaguzi, wanafunzi wote wanatarjiwa kuripoti haraka iwezekanavyo matukio ya ukiukaji wa kanuni za maadili mema kwa mwalimu, mtoa huduma ya ushauri, Mwalimu Mkuu wa Shule au mwakilishi wake. Mwanafunzi yeyote anayemwona mwanafunzi aliye na silaha, pombe au kitu kilichopigwa marufuku shuleni au katika shughuli ya shule anatarajiwa kuripoti habari hizi mara moja kwa mwalimu, Mwalimu Mkuu, mwakilishi wa Mwalimu Mkuu au Msimamizi Mkuu.

Wanafunzi wanakatazwa kutoa taarifa za uongo kimakusudi au kutoa habari za uongo kimakusudi kwa wafanyakazi wa shule wakati wa utaratibu wa kuchukuliwa kwa hatua ya adhabu.

Wafanyakazi wote wa wilaya walioidhinishwa kuchukua hatua za adhabu wanatarajiwa kufanya hivyo kwa njia ya haki, ya kisheria na haraka iwezekanavyo. Wafanyakazi wa wilaya ambao hawajaidhinishwa kuchukua hatua za adhabu wanatarajiwa kuripoti haraka iwezekanavyo matukio ya ukiukaji wa kanuni za maadili mema kwa msimamizi wao, ambaye kisha atachukua hatua ya adhabu inayofaa, ikiwa ameidhinishwa, au kuelekeza suala hilo kwa mfanyakazi aliyeidhinishwa kuchukua hatua inayofaa.

Silaha, pombe au kitu chochote kilichopigwa marufuku kinachopatikana kitachukuliwa mara moja, ikiwezekana kufuatiwa na ripoti kwa mzazi wa manafunzi anayehusika na kuchukuliwa kwa hatua za adhabu zinazofaa, ambazo zinaweza kujumuisha kufukuzwa kabisa shuleni na kushtakiwa ili kufunguliwa mashtaka.

Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima afahamishe shirika la eneo linalofaa la utekelezaji wa sheria kuhusu matukio hayo ya ukiukaji wa kanuni yanayosababisha kosa la kihalifu na kuathiri kwa kiwango kikubwa utulivu au usalama wa shule haraka iwezekanavyo, lakini haipaswi kuwa baada ya mwisho wa siku ambayo Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake anapata habari kuhusu tukio hilo la ukiukaji. Ripoti inaweza kuwasilishwa kwa simu, ikifuatwa na barua inayotumwa siku hiyo ambayo simu imepigwa. Ripoti hiyo lazima imtambulishe mwanafunzi na kueleza tabia iliyokiuka kanuni za maadili mema na kusababisha kosa la kihalifu.

**Usiri**

Ni sera ya wilaya kuheshimu usiri wa wahusika na mashahidi wote wanaohusika katika malalamiko ya ukiukaji wa Kanuni za Maadili Mema. Kadri iwezekanavyo, wilaya haitatoa maelezo ya malalamiko au utambulisho wa mlalamikaji au mtu/watu ambao malalamiko yamewasilishwa kuwahusu, kwa mtu mwingine yeyote ambaye hahitaji kujua maelezo hayo. Hata hivyo, kwa sababu hitaji la kudumisha usiri wa mtu lazima lisawazishwe na wajibu wa kisheria wa wilaya ili mshtakiwa ashughulikiwe kwa njia ya haki, kufanya uchunguzi wa kina au kuchukua hatua inayohitajika ili kusuluhisha malalamiko hayo, wilaya ina haki ya kutoa maelezo ya kuwatambulisha wahusika na mashahidi wanaohusika katika malalamiko hayo katika hali zinazofaa kwa watu wanaohitaji kujua. Mfanyakazi anayewajibika kwa kuchunguza malalamiko atajadili viwango vya usiri na wasiwasi wowote na wahusika wote katika malalamiko. Ikiwa mlalamikaji ataomba kuwa jina lake lisitambulishwe kwa mtu/watu ambao malalamiko yamewasilishwa kuwahusu, mfanyakazi anayewajibika kwa kufanya uchunguzi atamfahamisha mlalamikaji kuwa:

1. ombi hilo linaweza kuzuia uwezo wa wilaya wa kushughulikia malalamiko yake;
2. sera ya wilaya na sheria ya kitaifa inakataza kulipiza kisasi walalamikaji na mashahidi;
3. wilaya itajaribu kuzuia hali yoyote ya kulipiza kisasi; na
4. wilaya itachukua hatua kali ikiwa tukio la kulipiza kisasi litatokea.

Ikiwa bado mlalamikaji anaomba asitambulishwe baada ya kupewa taarifa ya hapo juu, mchunguzi atachukua hatua zote zinazofaa ili kuchunguza na kushughulikia malalamiko hayo kulingana na ombi hilo mradi kufanya hivyo hakuzuii wilaya kushughulikia ipasavyo matukio ya uchokozi kwa wengine.

# Tabia ya Mwanafunzi Inayokatazwa

Bodi inatambua haja ya kubainisha kwa uwazi na kwa njia maalum tabia inazotarajia kutoka kwa wanafunzi wakiwa shuleni au wanaposhiriki katika shughuli ya shule Kanuni za tabia zilizoelezwa hapa chini zinakusudiwa kufanya hivyo na kulenga usalama na kuheshimu haki na mali ya wengine. Wanafunzi ambao hawatakubali kuwajibika kwa tabia yao na wanaovunja kanuni hizi za shule watatakiwa kukubali matokeo ya tabia yao.

Wanafunzi wanaweza kuchukuliwa hatua ya adhabu, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, katika matukio mabaya zaidi au yanayojirudia, kufukuzwa shuleni kwa muda, wanapo:

A. Husika katika tabia isiyofaa. Mifano ya tabia ya aina hii ni pamoja na, lakini si tu:

1. Kukimbia au vinginevyo tabia isiyo salama kwenye njia za ukumbi.
2. Kupiga kelele bila sababu.
3. Kutumia lugha au ishara ambazo ni chafu, za kukera, za ukosefu wa adabu au za matusi.
4. Kuzuia njia ya magari au wanaotembea kwa miguu.
5. Kuhusika katika kitendo chochote cha kimakusudi kinachovuruga shughuli za kawaida za jamii ya shule, ikijumuisha kutoa taarifa za uongo kimakusudi.
6. Kuingia mahali bila ruhusa. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia katika jengo lolote shuleni, isipokuwa jengo wanaloingia kila mara, bila ruhusa kutoka kwa msimamizi anayesimamia jengo hilo.
7. Utumiaji mbaya wa kompyuta/mawasiliano ya kielektroniki, ikijumuisha utumiaji wowote ambao haujaidhinishwa wa kompyuta, programu au intaneti/akaunti ya intranet; kuingia kwenye tovuti ambazo hazifai; au uvunjaji mwingine wowote wa sera ya wilaya ya matumizi yanayokubalika.

B. Kuhusika katika tabia ya kikaidi. Mifano ya tabia ya aina hii inajumuisha kuhusika katika tabia inayokiuka kimakusudi jambo ambalo mwanafunzi ameambiwa afanye au mahali ambapo anapaswa kuwa wakati wowote. Tabia hii inachukuliwa kuwa ukaidi. Mifano ya tabia ya aina hii ni pamoja na, lakini si tu:

1. Kukosa kufuata maelekezo ya busara ya walimu, wasimamizi wa shule au wafanyakazi wengine wa shule wanaosimamia wanafunzi au vinginevyo kuonyesha tabia ya uchokozi au ukosefu wa heshima.
2. Kuchelewa, kukosa au kuondoka shuleni bila ruhusa.
3. Kukwepa kizuizi.

C. Kuhusika katika tabia ya kuvuruga. Mifano ya tabia ya aina hii inajumuisha kuhusika katika tabia inayozuia wengine kuweza kujifunza, kumakinika au kufanya kazi yao. Tabia hii inachukuliwa kuwa ya kuvuruga. Mifano ya tabia ya aina hii ni pamoja na, lakini si tu:



1. Tabia ya wazi ya kingono isiyofaa.
2. Kuonyesha au utumiaji wa vifaa binafsi vya kielektroniki, kama vile, lakini si tu, simu za mkononi, vicheza muziki au video, kamera, kwa njia inayokiuka sera ya wilaya.

D. Kuhusika katika tabia ya vurugu. Mifano ya tabia ya aina hii ni pamoja na, lakini si tu:

1. Kutenda kitendo cha vurugu (kama vile kugonga, kupiga teke, kupiga ngumi na kukwaruza) kwa mwalimu, msimamizi, mfanyakazi mwingine wa shule, mwanafunzi mwingine au mtu mwingine yeyote aliye shuleni kisheria.
2. Kuwa na silaha. Maafisa wa utekelezaji wa sheria walioidhinishwa ndio watu pekee wanaoruhusiwa kuwa na silaha shuleni au katika shughuli ya shule.
3. Kuonyesha kitu kinachoonekana kuwa silaha.
4. Kutishia kutumia silaha yoyote.
5. Kuharibu kimakusudi mali binafsi ya mwanafunzi, mwalimu, msimamizi, mfanyakazi mwingine wa wilaya au mtu mwingine aliye shuleni kisheria, ikijumuisha grafiti au kuchoma kwa moto.
6. Kuharibu kimakusudi mali ya wilaya ya shule.

E. Kuhusika katika tabia yoyote inayohatarisha usalama, afya ya mwili au ya kihisia au ustawi wa wengine. Mifano ya tabia ya aina hii ni pamoja na, lakini si tu:

1. Kujaribu kuhusika au kutenda kitendo cha vurugu kilichoelezwa katika Kifungu cha D.
2. Kuhatarisha wanafunzi wengine, wafanyakazi wa shule au mtu mwingine yeyote aliye shuleni au anayehudhuria shughuli ya shule kwa kujihusisha kiholela katika tabia inayosababisha hatari kubwa ya kusababisha jeraha la mwili.
3. Kuiba au kujaribu kuiba mali ya wanafunzi wengine, wafanyakazi wa shule au mtu mwingine yeyote aliye shuleni kisheria au anayehudhuria shughuli ya shule.
4. Kuharibia jina, inayojumuisha kutoa taarifa za uongo au ambazo hazijathibitishwa au kutoa taarifa kuhusu mtu binafsi au kikundi kinachotambulika zinazoharibu sifa ya mtu au kikundi kinachotambulika kwa kuwadhalilisha.
5. Ubaguzi, inayojumuisha kutumia asili (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, imani, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, jinsia (utambulisho na mwonekano), mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi, uzito au ulemavu kunyima haki, usawa au utumiaji wa vifaa vinavyotumiwa na wengine.
6. Usumbufu (au Uchokozi), ni kusababisha mazingira ya uadui kwa tabia au vitisho, kutishia au kudhulumu. (Angalia sera ya 0115, Kuchukua Hatua na Uzuiaji wa Uchokozi na Usumbufu wa Mwanafunzi ili upate ufafanuzi kamili.)
7. Kutishia, inayojumuisha kuhusika katika vitendo au kutoa kauli zinazomfanya mtu kuhofia kudhuriwa kimwili.
8. Uaibishaji, inayojumuisha utaratibu wa kutambulishwa, kuapishwa au kufanywa kuwa mshirika unaohusisha vitendo vya usumbufu (angalia sera ya 0115 ili upate ufafanuzi kamili).
9. Kuuza, kutumia, kusambaza au kumiliki vitu vilivyopigwa marufuku.
10. Kutumia lugha isiyo ya adabu au ya matusi, kulaani au kuapa.
11. Kuvuta sigara, biri, bomba, sigara ya kielektroniki (yaani, vape), au kutumia tumbaku ya kutafunwa au isiyotoa moshi, au kuvuta moshi/ mvuke/kula bangi au bangi iliyosindikwa (ikijumuisha bidhaa za bangi) au kuvuta katani ya bangi (isipokuwa kwa matumizi ya kisheria ya matibabu ya bangi kulingana na sheria na kanuni za jimbo).
12. Kumiliki, kutumia, kuuza, kutoa, kutengeneza, kusambaza au kubadilishana vinywaji vya pombe au dawa zilizopigwa marufuku, au kulewa kutokana na mojawapo ya vitu hivyo. "Dawa zilizopigwa marufuku" ni pamoja na, lakini si tu, dawa za kuvuta hewa yake, bangi, kokeini, LSD, PCP, amfetamini, heroini, dawa za kusisimua misuli, mifano ya dawa, na dawa zozote zilizotengenezwa kutokana na kemikali, iwe zimepigwa marufuku moja kwa moja au la, zinazojulikana kwa kawaida kama "designer drugs" ambazo ni dawa zilizobuniwa na kutengenezwa ili kuiga athari na matumizi yanayokusudiwa, ambazo zina kiwango kikubwa cha usawa wa kemikali na dawa zilizopigwa marufuku, ambazo zinaweza kuwa au zisiwe na lebo ya kuruhusiwa kutumiwa na binadamu.
13. Kutumia vibaya au kutumia pamoja dawa zilizoagizwa na daktari na dawa za kununua dukani bila maagizo ya daktari.
14. Kucheza kamari.
15. Kuona vitu vichafu, yaani, kuona sehemu za siri za mwili kwa njia ya kukera au isiyofaa.
16. Kupiga ripoti ya onyo la mkasa wa moto au mkasa mwingine bila sababu nzuri, utumiaji mbaya wa simu ya 911, au kufungua mtungi wa kuzima moto.
17. Kutoa taarifa za uongo kimakusudi au kutoa habari za uongo kimakusudi kwa wafanyakazi wa shule wakati wa utaratibu wa kuchukuliwa kwa hatua ya adhabu.

F. Kuhusika katika tabia zisizofaa zinazokatazwa katika vifungu vya A hadi E vya kifungu hiki ukiwa kwenye basi la shule na kubaki kwenye kiti chako, kutorusha vitu na mikono na miguu ndani ya basi, kufuata maelekezo ya dereva wa basi au makanga. Ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na tabia njema wakiwa kwenye mabasi ya wilaya, ili kuhakikisha usalama wao na wa abiria wengine na kuepuka kumfanya dereva akose kumakinika. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na tabia njema kwenye basi kwa njia inayolingana na viwango vilivyowekwa vya tabia ya darasani. Tabia za kupiga kelele kupita kiasi, kusukumana, kupigana kumbo na kupigana hazitaruhusiwa.

G. Kuhusika katika aina yoyote tabia ya kielimu isiyofaa. Mifano ya tabia ya kielimu isiyofaa ni pamoja na, lakini si tu:

1. Kuiba kazi ya wengine: Hii inafafanuliwa kama kitendo cha kuiba au kuwasilisha mawazo au maneno ya mtu mwingine kuwa ni yako binafsi, au kutumia chapisho liliotayarishwa bila kutambua chanzo chake. Hii inajumuisha mawazo au maneno kutoka kwa chapisho lolote na/au intaneti. Wanafunzi lazima watumie mitajo na marejeleo yanayofaa wanapotumia kazi au mawazo ya mtu mwingine.
2. Udanganyifu Wilaya inatambua sera na taratibu zote zinazohitajika na NYSED kwa matukio ya udanganyifu katika Mitihani yote ya Jimbo la New York. Wanafunzi hawapaswi kupeana au kupokea taarifa, ikijumuisha kielektroniki, kwa aina yoyote ya jaribio, maswali, kazi ya kufanyia nyumbani, kazi ya shuleni au kazi ya maabara.
3. Kunakili, Kudanganya au Kubuni: Kudanganya inarejelea kitendo cha kubadilisha, kuongeza au kufuta maelezo au kutoa kimakusudi maelezo ya uongo/yasiyo sahihi. Ubunifu inarejelea kitendo cha kutoa nakala au kuiga hati kwa makusudi ya kudanganya.
4. Kubadilisha rekodi: Kubadilisha rekodi inafafanuliwa kama kubadilisha au kurekebisha rekodi yoyote inayohusiana na mwanafunzi.
5. Kumsaidia mwanafunzi mwingine kufanya vitendo vyovyote vya hapo juu.

H. Kuhusika katika tabia isiyofaa nje ya shule inayoathiri au inayoweza kutarajiwa kuvuruga kwa kiwango kikubwa utaratibu wa elimu shuleni au katika shughuli ya shule. Tabia hiyo isiyofaa ni pamoja na, lakini si tu, kutishia au kusumbua wanafunzi au wafanyakazi wa shule kupitia njia yoyote nje ya shule, ikijumuisha uchokozi wa mtandaoni (ili upate ufafanuzi kamili wa usumbufu, uchokozi na uchokozi wa mtandaoni rejelea sera ya 0115, Kuchukua Hatua na Uzuiaji wa Uchokozi na Usumbufu wa Mwanafunzi.

# Kanuni za Mavazi ya Mwanafunzi

Wanafunzi wote wanatarajiwa kuzingatia zaidi usafi wa mwili na kuvalia mavazi yanayofaa shuleni na katika shughuli za shule. Wanafunzi na wazazi wao wana jukumu kuu la kuhakikisha mavazi na mwonekano wa mwanafunzi unaokubalika. Walimu na wafanyakazi wengine wote wa wilaya wanapaswa kuwa mfano na kusisitiza mavazi ya mwanafunzi yanayokubalika na kuwasaidia wanafunzi kuelewa mwonekano unaofaa shuleni.


Mavazi ya mwanafunzi, usafi na mwonekano, ikijumuisha mtindo wa nywele/rangi, mapambo, mipako ya urembo na kucha, lazima:

1. Yasiwe na uwezekano wa kuwaumiza watu au kuharibu mali, yafae kulingana na kanuni hii, na hayapaswi kuvuruga kwa kiwango kikubwa au kuathiri zaidi utaratibu wa kielimu.
2. Watambue kuwa nguo fupi zaidi na nguo nyepesi zinazoonyesha mwili hazifai.
3. Wahakikishe kuwa mavazi ya ndani yamefunikiwa na nguo ya juu. (mikanda na kamba za kiunoni zinazoonekana si kosa)
4. Wavae viatu wakati wote. Viatu vinavyosababisha hatari kwa usalama havitaruhusiwa.
5. Wanafunzi wanapaswa kutambulika kwa urahisi wakati wote, isipokuwa kwa makusudi ya kimatibabu au kidini, nguo inapaswa kuvaliwa kwa njia ambayo haifuniki zaidi uso au kuzuia mtu kutambulika.
6. Hayapaswi kuwa na vitu vya kuonyesha ukosefu wa adabu, vichafu, vya kukashifu au vya kupaka tope, vya kusumbua au kubagua wengine kulingana na asili (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo), rangi, dini, imani, taifa la asili, kabila, jinsia, (ikijumuisha utambulisho na mwonekano wa kijinsia), mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi au ulemavu. 7. Hayapaswi kuhimiza na/au kupendekeza utumiaji wa pombe, tumbaku au dawa zinazodhibitiwa au dawa zilizopigwa marufuku na/au kuhimiza shughuli nyingine za kinyume cha sheria au za vurugu.

Hakuna chochote katika sera hii kinachopaswa kueleweka kuwa kinazuia uwezo wa wanafunzi kuonyesha utambulisho wao wa kijinsia kupitia mavazi, mapambo, mipako ya urembo au rangi au mitindo ya kucha au kuwaadhibu wanafunzi kwa kufanya hivyo. Vilevile, hakuna chochote katika sera hii kinachopaswa kueleweka kuwa kinawazuia wanafunzi kuweka mitindo ya nywele inayoonyesha sifa inayohusishwa kihistoria na asili yao (kama vile hali na mitindo ya nywele ya kujilinda kama vile misuko, misokoto na mikunjo) au kuwaadhibu kwa kufanya hivyo.

Kila Mwalimu Mkuu wa Shule au mwakilishi wake atawajibika kwa kuwafahamisha wanafunzi wote na wazazi wa wanafunzi kuhusu kanuni za mavazi ya mwanafunzi mwanzoni mwa mwaka wa shule na marekebisho yoyote yanayofanywa kwenye kanuni za mavazi katika mwaka wa shule.

Utekelezaji wa kanuni hizi za mavazi lazima ufanyike kwa busara na kwa umakinifu mkubwa, kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kufikia uwezo wao kamili, si kuwaabisha au kuwashtumu, na kupunguza uharibu wa muda wa mafunzo. Wafanyakazi, hasa wale walio na uhusiano mzuri na mwanafunzi, wanatarajiwa kushughulikia matukio ya ukiukaji wa kanuni za mavazi na wanafunzi husika kwa siri, kutambua kama kuna sababu zinazoathiri uwezo wa mwanafunzi wa kufuata kanuni za mavazi na kusaidia kushughulikia masuala hayo. Wanafunzi ambao mwonekano wao unakiuka kanuni za mavazi ya mwanafunzi watatakiwa kurekebisha mwonekano wao kwa kufunika au kuondoa kitu kinachokera, na ikiwa inahitajika au inawezekana, kukibadilisha na kitu kinachokubalika. Mwanafunzi yeyote anayekataa kufanya hivyo anaweza kuadhibiwa, mwanafunzi anayekosa kufuata kanuni za mavazi mara kwa mara anaweza kuadhibiwa zaidi.



# Adhabu, Tarartibu na Maelekezo

Ni muhimu kutofautisha kati ya tabia ndogo zinazoweza kudhibitiwa na wafanyakazi wanaoshirikiana kwa karibu zaidi na mwanafunzi na tabia kubwa zinazopaswa kudhibitiwa na msimamizi. Maelezo yaliyo hapa chini yanatoa mwongozo wa tabia hizo pamoja na hatua ambazo wafanyakazi wanaweza kuchukua ili kushughulikia tabia hizi.

| **Tabia Ndogo** | **Tabia Kubwa** |
|---|---|
| Kukataa kufuata maelekezo/kufanya kazi, ukaidi | Makosa madogo ya mara kwa mara |
| Kutokuwa tayari | Kuwa na silaha |
| Kujibizana, kukosea heshima wafanyakazi na wenzake | Kutumia majina ya matusi |
| Kuzungumza zaidi, kuvuruga mafunzo | Uchokozi/usumbufu |
| Kubishana na mtu mzima au mwenzake (sauti/hisia) | Kupigana |
| Kugusa | Vitendo vya uchokozi |
| Kuchelewa | Utumiaji wa dawa za kulevya/pombe |
| Utumiaji mbaya wa vifaa vya kielektroniki | Shughuli ya kingono au shughuli ya kingono isiyofaa |
| Lugha isiyofaa | Mwanafunzi kutoroka shule (kuondoka shuleni bila ruhusa |
| Kutokuwa mwaminifu | Uharibifu wa mali |
| Ukiukaji wa kanuni za mavazi | Wizi/udanganyifu |

**Hatua za Kudhibiti Tabia Ndogo**

Tabia nyingi ndogo zinapaswa kudhibitiwa na wafanyakazi wanaoshirikiana kwa karibu zaidi na mwanafunzi.

**Hatua za darasani:**

**Hatua ya 1:** Kuelekeza upya, kueleza upya matarajio, kutoa msaada wa ziada ikiwa unahitajika

Tabia hiyo ikiendelea, nenda kwenye hatua ya 2. Tabia hiyo ikoma, tambua hilo kwa kusifia tabia maalum

**Hatua ya 2:** Kuonya kwa Matamshi: eleza upya tabia inayotarajiwa, eleza unachotaka kuona hasa na kwamba tabia hiyo inatakiwa kukoma na hatua maalum zitakazochukuliwa ikiwa itaendelea

Tabia hiyo ikiendelea, nenda kwenye hatua ya 3. Tabia hiyo ikoma, tambua hilo kwa kusifia tabia maalum

**Hatua ya 3:** Mfanyakazi Anachukua Hatua: kufanya mkutano na mwanafunzi kwa siri, kubadilisha mahali pa kukaa, kuwasiliana na mzazi, kupoteza haki, kupelekwa katika darasani la mwalimu mwingine ili kupumzika kidogo (kubadilisha mazingira), kurejeshwa darasani

Tabia hiyo ikiendelea, nenda kwenye hatua ya 4. Tabia hiyo ikoma, tambua hilo kwa kusifia tabia maalum

**Hatua ya 4:** Ikiwa hatua zote za hapo juu hazijabadilisha tabia hiyo, omba mkutano wa kumsaidia mwanafunzi (timu ya data) ili kubuni mpango mzuri wa hatua za kuchukua au misaada mingine ya kukuza ujuzi unaohitajika

**Hatua za Kudhibiti Tabia Kubwa**

Tabia nyingi kubwa zinapaswa kudhibitiwa na msimamizi.

**Hatua ya 1:** Hakikisha kuwa kila mtu yuko salama. Ondoka katika eneo hilo, ikiwa inahitajika.

**Hatua ya 2:** Mwite msimamizi akusaidie na utumie mikakati ya utulizaji.

**Hatua ya 3:** Jaza fomu ya ripoti ya tabia.

**Hatua ya 4:** Msimamizi anafanya uchunguzi na kuchukua hatua, inavyohitajika.

**Hatua ya 5:** Kurejea baada ya kurekebisha tabia au mkutano wa kukaribishwa tena unafanyika na kuweka lengo.

Ingawa huenda kukawa na hatua nyingi za kawaida za kuchukuliwa pamoja na mafunzo ya tabia inayotarajiwa na kuchukulia masuala ya adhabu kama matukio ya mafunzo, hii ni mbinu bora zaidi kuliko tu kushughulikia matukio husika isipokuwa tabia za mwanafunzi ziwe zinasababisha hatari ya moja kwa moja au endelevu kwa usalama wa wanafunzi wengine na wafanyakazi. Kwa hivyo, bodi inaidhinisha mbinu za urekebishaji zitumike panapofaa. Mbinu hii inalenga uwajibikaji wa papo hapo na mabadiliko ya tabia. Jambo muhimu kwa utekelezaji wa mbinu za hatua za urekebishaji ni kuwasaidia wanafunzi ambao wamehusika katika tabia isiyokubalika:

- Waelewe kwa nini tabia hiyo haikubaliki na madhara iliyosababisha;
- Waelewe kile ambacho wangefanya tofauti katika hali hiyo;
- kuwajibika kwa vitendo vyao;
- Wapewe fursa ya kujifunza mikakati/ujuzi wa kujenga mahusiano mazuri wa kutumia baadaye; na
- Waelewe kuwa hatua kali zaidi za adhabu zinaweza kuchukuliwa ikiwa tabia hiyo itatokea tena.

Hatua za kuchukuliwa, na ikihitajika adhabu, husaidia zaidi vinaposhughulikia tatizo moja kwa moja wakati na mahali linapotokea, na kwa njia ambayo wanafunzi wanaona kuwa ni ya haki na isiyoegemea upande wowote. Wafanyakazi wa shule wanaoshirikiana na wanafunzi wanatarajiwa kutumia hatua ya adhabu panapohitajika tu na kusisitiza uwezo wa wanafunzi wa kukuza nidhamu yao.

Hatua za kuchukuliwa na hatua ya adhabu, zinapohitajika, zinapaswa kuwa kali, za haki na zisizobadilika ili zisaidie zaidi kubadilisha tabia ya mwanafunzi. Katika kutambua hatua ya adhabu inayofaa, wafanyakazi wa shule walioidhinishwa kuchukua hatua za adhabu watazingatia yafuatayo:

1. Umri wa mwanafunzi.
2. Hali ya kosa na hali zilizosababisha kosa hilo.
3. Rekodi ya awali ya nidhamu ya mwanafunzi.
4. Ufaafu wa aina nyinginezo za adhabu.
5. Maelezo kutoka kwa wazazi, walimu na/au watu wengine, panapofaa.
6. Hali nyingine za kupunguza ukali wa adhabu.

Kama kanuni ya jumla, ukali wa adhabu utakuwa na viwango. Hii inamaanisha kwamba kwa kawaida kosa la kwanza la mwanafunzi halitachukuliwa hatua kali kuliko makosa ya baadaye. Hata hivyo, wafanyakazi wa wilaya wamepewa uwezo wa kutumia hatua inayofaa zaidi iliyopimwa ya kuhakikisha mwanafunzi anajifunza kutokana na tabia yake na kujihusisha na tabia ya kujenga mahusiano mazuri zaidi baadaye.

Ikiwa tabia ya mwanafunzi inahusiana na ulemavu au ulemavu unaoshukiwa, mwanafunzi huyo ataelekezwa kwa Kamati kuhusu Elimu Maalum na adhabu, ikiwa inahitajika, itatolewa kulingana na mahitaji tofauti ya kanuni hizi za maadili mema za kuadhibu wanafunzi wenye ulemavu au wanaodhaniwa kuwa na ulemavu. Mwanafunzi anayetambuliwa kuwa na ulemavu hataadhibiwa kwa tabia inayohusiana na ulemavu wake, isipokuwa adhabu hiyo iwe inalingana na mpango binafsi wa elimu ya mwanafunzi (Individualized Education Plan, IEP).

### A. Hatua za kuchukuliwa

Bodi inatarajia kutumika kwa mbinu zinazowaruhusu waalimu kushughulikia masuala ya adhabu kama fursa za mafunzo badala ya kuadhibu panapofaa, badala ya kutegemea viwango tofauti vya adhabu. Wanapochagua vitendo na hatua za kuchukuliwa kuhusu tabia ya mwanafunzi, mwalimu, wasimamizi na wafanyakazi lazima wasawazishe malengo mawili ya wilaya ya kukomesha uvurugaji wa shule na kutumia vyema muda mafunzo ya mwanafunzi.

Wanafunzi wanaopatikana kuwa wamehusika katika tabia isiyofaa wanaweza kuchukuliwa hatua na vitendo vifuatavyo, labda peke yake au kwa pamoja. Mfanyakazi wa shule aliyetengwa kushughulikia kila hatua ana idhini ya kuchukua hatua hiyo, kulingana na haki ya mwanafunzi ya kukata rufaa.

1. Kuonywa kwa matamshi - mkutano wa mwalimu/mwanafunzi, kuwasiliana na mzazi, kusimamisha darasani kwa muda, kuondolewa darasani kwa muda, kupoteza haki za darasani - mfanyakazi yeyote wa wilaya
2. Kuonywa kwa maandishi – madereva wa basi, wasimamizi wa ukumbi na chakula cha mchana/mapumziko, makocha, watoa huduma ya ushauri, walimu, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
3. Kutuma taarifa ya onyo kwa mzazi – dereva wa basi, wasimamizi wa ukumbi na chakula, makocha, watoa huduma ya ushauri, walimu, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
4. Kuzuiliwa – walimu, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
5. Kusimamishwa kusafirishwa – Msimamizi wa Usafiri, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu




6. Kusimamiwa kushiriki katika michezo – Msimamizi wa Michezo, Makocha, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
7. Kusimamishwa kushiriki katika shughuli ya kijamii au za nje ya masomo – msimamizi wa shughuli, Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
8. Kusimamishwa kwa haki nyinginezo – Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
9. Kusimamishwa kuhudhuria madarasa – Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu
10. Kuondolewa darasani na Mwalimu – Mwalimu, Mwalimu Mkuu
11. Kusimamishwa shule kwa muda mfupi (siku tano au chache) – Mwalimu Mkuu, Msimamizi Mkuu, Bodi ya Elimu
12. Kusimamishwa shule kwa muda mrefu (siku tano au zaidi) – Msimamizi Mkuu, Bodi ya Elimu
13. Kusimamishwa shule kabisa – Msimamizi Mkuu, Bodi ya Elimu

**B. Taratibu**

Kiwango cha rufaa ambayo mwanafunzi ana haki ya kukata kabla ya hatua kuchukuliwa kinalingana na hatua inayochukuliwa. Katika kesi zote, bila kujali hatua iliyochukuliwa, mfanyakazi wa shule aliyeidhinishwa kuchukua hatua lazima amfahamishe mwanafunzi kuhusu tabia isiyofaa inayodaiwa na lazima achunguze, kadri iwezekanavyo, maelezo yanayohusiana na tabia hiyo isiyofaa inayodaiwa. Wanafunzi wote watakuwa na fursa ya kujitetea kwa mfanyakazi wa shule anayechukua hatua ya adhabu kuhusiana na hatua ya adhabu inayochukuliwa.

Wanafunzi wanaopaswa kuchukuliwa hatua isiyo ya kuonywa kwa matamshi, kuonywa kwa maandishi au kutumwa kwa taarifa ya onyo kwa wazazi wao wana haki za ziada kabla ya kuchukuliwa kwa hatua hiyo. Haki hizi za ziada zimeelezwa hapa chini:

1. **Kuzuiliwa:** Walimu, Mwalimu Mkuu na Msimamizi Mkuu wanaweza kutumia hatua ya kuzuiliwa baada ya shule kama hatua ya kuchukuliwa kwa tabia ya mwanafunzi katika hali ambapo hatua ya kuondolewa darasani au kusimamishwa shule haifai. Kuzuiliwa kutatumika kama hatua ya kuchukuliwa baada tu ya mzazi wa mwanafunzi kutumiwa taarifa ya kuthibitisha kuwa hakuna pingamizi kutoka kwa mzazi ya kuchukuliwa kwa hatua hiyo na mwanafunzi ana huduma inayofaa ya kusafiri kwenda nyumbani baada ya kuzuiliwa.
2. **Kusimamishwa kusafirishwa**: Wanafunzi wasipokuwa na tabia njema kwenye basi, dereva wa basi anatarajiwa kuripoti tabia hiyo isiyofaa kwa Mwalimu Mkuu. Wanafunzi wanaokuwa tatizo kubwa la kinidhamu haki zao za kusafiri kwenye basi zinaweza kusimamishwa na Mwalimu Mkuu au Msimamizi Mkuu au mwakilishi wake. Katika hali hizo, mzazi wa mwanafunzi huyo atawajibikia usafiri wa mtoto wake wa kwenda na kutoka shuleni salama. Iwapo hali ya kusimamishwa kusafirishwa itasababisha kusimamishwa shule, wilaya itaweka mpango unaofaa wa kuhakikisha mwanafunzi huyo anapata elimu.

Mwanafunzi anayesimamishwa kusafirishwa hana haki ya kesi yake kusikilizwa kikamilifu kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha §3214. Hata hivyo, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa fursa inayofaa ya kufanya mkutano usio rasmi na Mwalimu Mkuu, ili kujadili tabia iliyofanyika na hatua iliyochukuliwa.

3. **Kusimamishwa kushiriki katika michezo, shughuli za nje ya elimu ya darasani na haki nyingine**: Mwanafunzi anayesimamishwa kushiriki katika michezo, shughuli za nje ya elimu ya darasani au haki nyinginezo hana haki ya kesi yake kusikilizwa kikamilifu kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha §3214. Hata hivyo, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa fursa inayofaa ya kufanya mkutano usio rasmi na afisa wa wilaya aliyechukua hatua ya kumsimamisha ili kujadili tabia iliyofanyika na hatua iliyochukuliwa.

4. **Kusimamishwa Kuhudhuria Madarasa**: Bodi inatambua kuwa shule lazima isawazishe haja ya mwanafunzi ya kuhudhuria shule na haja ya kuwa na utulivu darasani ili kuwezesha mazingira mazuri ya mafunzo. Kwa hivyo, Bodi inawapa idhini Walimu Wakuu na Msimamizi Mkuu au mwakilishi wake kuchukua hatua ya 'kusimamishwa kuhudhuria madarasa' kwa wanafunzi ambao vinginevyo wangepaswa kusimamishwa shule kwa sababu ya uvunjaji wa kanuni za maadili mema. Mwalimu wa kuchukua hatua ya kusimamishwa kuhudhuria madarasa atakuwa mwalimu aliyeidhinishwa.

Mwanafunzi anayesimamishwa kuhudhuria madarasa hana haki ya kesi yake kusikilizwa kikamilifu kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha §3214. Hata hivyo, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa fursa inayofaa ya kufanya mkutano usio rasmi na afisa wa wilaya aliyechukua hatua ya kumsimamisha kuhudhuria madarasa ili kujadili tabia iliyofanyika na hatua iliyochukuliwa.

5. **Hatua ya Adhabu Inayochukuliwa na Mwalimu ya Kuwaondoa Wanafunzi Wanaovuruga Mafunzo:** Tabia ya mwanafunzi inaweza kuathiri uwezo wa mwalimu wa kufunza na inaweza kufanya iwe vigumu kwa wanafunzi wengine darasani kujifunza. Mara nyingi mwalimu wa darasani anaweza kudhibiti tabia ya mwanafunzi na kudumisha au kurejesha udhibiti wa darasa kwa kutumia mbinu nzuri za udhibiti wa darasa. Mbinu hizi zinaweza kujumuisha mbinu zinazohusisha mwalimu kumwamuru

mwanafunzi aondoke darasani kwa muda ili kumpa mwanafunzi fursa ya kutulia na kujidhibiti katika mazingira tofauti. Mbinu hizo zinaweza kuwa ni pamoja na, lakini si tu:

1. 'Kupumzika' kwa muda mfupi kwenye darasa la msingi au kwenye ofisi ya msimamizi
2. Kumwamuru mwanafunzi asimame nje ya darasa kwa muda mfupi
3. Kumwamuru mwanafunzi aende kwenye ofisi ya Mwalimu Mkuu kwa muda wa darasa uliosalia pekee
4. Kumwamuru mwanafunzi aende kwa mtoa huduma ya ushauri au mfanyakazi mwingine wa wilaya ili apewe ushauri.

Mbinu za udhibiti wa darasa zinazozingatia muda kama hizi hazichukuliwei kama adhabu za kuondolewa darasani kwa makusudi ya kanuni hizi. Walimu kwanza watatumia mbinu zinazolenga kufunza tabia zinazofaa na za uwajibikaji ili wanafunzi waweze kujifunza na kuwa na tabia za kielimu, kijamii na kihisia ambazo ni salama na zenye heshima. Mifano ya mbinu hizi inajumuisha kutumia kauli zinazofaa, kutumia maswali ya kuhimiza kujieleza, kuanzisha uhusiano mzuri na wanafunzi, kupeana maelekezo mazuri yanayoeleza matarajio na kutoa maoni mazuri na maalum.

Wakati mwingine, tabia ya mwanafunzi inaweza kuwa sumbufu zaidi kuliko mwalimu anavyoweza kutarajia. Kwa makusudi ya kanuni hizi za maadili mema, mwanafunzi msumbufu ni mwanafunzi ambaye anavuruga zaidi utaratibu wa elimu au anayeathiri zaidi uwezo wa mwalimu wa kudhibiti darasa. Hali ya kuvuruga zaidi utaratibu wa elimu au kuathiri zaidi uwezo wa mwalimu hutoka wakati mwanafunzi anakataa mara kwa mara kufuata maagizo ya mwalimu au kuvunja mara kwa mara kanuni za darasani za mwalimu.

Mwalimu wa darasani anaweza kumwondoa darasani mwanafunzi msumbufu hadi siku mbili. Hatua ya kuondolewa darasani inahusiana na darasa la mwalimu aliyemwondoa mwanafunzi darasani pekee.

Ikiwa mwanafunzi msumbufu hasababishi hatari au tishio la kuendelea kuvuruga utaratibu wa elimu, mwalimu lazima ampe mwanafunzi maelezo ya sababu ya kuondolewa kwake darasani na fursa ya kujitetea kuhusiana na matukio husika kabla ya mwanafunzi huyo kuondolewa darasani. Ni baada tu ya majadiliano yasiyo rasmi ndipo mwalimu anaweza kumwondoa mwanafunzi darasani.

Ikiwa mwanafunzi anasababisha hatari au tishio la kuendelea kusumbua, mwalimu anaweza kuamrisha mwanafunzi huyo aondolewe darasani mara moja. Hata hivyo, mwalimu lazima amweleze mwanafunzi huyo sababu ya kuondolewa kwake darasani na kumpa mwanafunzi fursa ya kujitetea kuhusiana na matukio husika ndani ya saa 24 za wiki ya kazi.

Mwalimu lazima ajaze fomu ya wilaya ya adhabu ya kuondolewa darasani na akutane na Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake haraka iwezekanavyo, lakini isiwe baada ya mwisho wa siku ya shule, ili kueleza hali zilizosababisha kuondolewa kwa mwanafunzi darasani na kuwasilisha fomu ya adhabu ya kuondolewa darasani. Ikiwa Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake hayupo kufikia mwisho wa siku hiyo ya shule, mwalimu lazima amwachie katibu fomu hiyo na akutane na Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake kabla ya kuanza kwa madarasa siku ya shule inayofuata.

Ndani ya saa 24 baada ya mwanafunzi kuondolewa darasani na katika wiki ya kazi, Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima amfahamishe mzazi wa mwanafunzi huyo, kwa maandishi, kuwa mwanafunzi ameondolewa darasani na sababu ya kuondolewa. Taarifa hiyo lazima pia imfahamishe mzazi kuwa ana haki, akiomba, ya kufanya mkutano usio rasmi na Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake ili kujadili sababu za mwanafunzi kuondolewa darasani.

Taarifa hiyo ya maandishi lazima iwasilishwe na mtu, au kwa njia nyingine iliyotathmini ipasavyo ili kuhakikisha taarifa hiyo inapokewa ndani ya saa 24 baada ya mwanafunzi kuondolewa darasani na katika wiki ya kazi, kwa anwani inayojulikana ya mzazi. Panapowezekana, taarifa hiyo inapaswa kuwasilishwa kwa simu ikiwa shule imepewa namba ya/za simu kwa makusudi ya kuwasiliana na wazazi. Mwalimu Mkuu anaweza kumwomba mwalimu aliyeamrisha kuondolewa kwa mwanafunzi darasani ahudhurie mkutano huo usio rasmi.

Ikiwa katika mkutano huo usio rasmi mwanafunzi atakana mashtaka, Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima aeleze kwa nini mwanafunzi aliondolewa darasani na kumpa mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo fursa ya mwanafunzi kujitetea kuhusiana na matukio husika. Mkutano huo usio rasmi lazima ufanyike ndani ya saa 48 na katika wiki ya kazi, baada ya mwanafunzi kuondolewa darasani. Wakati wa kufanyika kwa mkutano huo usio rasmi unaweza kuongezwa kwa makubaliano ya mzazi na Mwalimu Mkuu.

Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake anaweza kutendua hatua ya kuondolewa kwa mwanafunzi darasani ikiwa atatambua mojawapo ya yafuatayo:

1. Hakuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha mashtaka yanayomhusu mwanafunzi.
2. Hatua hiyo ya kumwondoa mwanafunzi darasani inakiuka sheria, ikijumuisha kanuni za maadili mema za wilaya.
3. Tabia hiyo inasababisha mwanafunzi kusimamishwa shule kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha §3214 na hatua ya kusimamishwa shule itachukuliwa.

Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake anaweza kutendua hatua ya mwanafunzi kuondolewa darasani wakati wowote kati ya wakati wa kupokea fomu ya rufaa iliyowasilishwa na mwalimu na mwisho wa siku ya kazi katika kipindi cha saa 48 na katika wiki ya kazi baada ya kufanyika kwa mkutano usio rasmi. Hakuna mwanafunzi aliyeondolewa darasani na mwalimu wa darasa atakayeruhusiwa kurudi darasani hadi uamuzi wa mwisho utakapofanywa au hadi kipindi cha kuondolewa darasani kitakapoisha, chochote kitakachotangulia.

Mwanafunzi yeyote msumbufu aliyeondolewa darasani na mwalimu wa darasa atapewa shughuli na mpango wa kuendelea na elimu

yake hadi atakaporuhusiwa kurudi darasani.

Kila mwalimu lazima aweke kumbukumbu kamili (kwenye fomu ya wilaya) ya matukio yote ya kuondolewa kwa wanafunzi kwenye darasa lake. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima aweke kumbukumbu ya matukio yote ya kuondolewa kwa wanafunzi darasani.

Kuondolewa darasani kwa mwanafunzi mwenye ulemavu, chini ya hali fulani, kunaweza kusababisha kubadilishwa kwa darasa la mwanafunzi huyo. Vilevile, hakuna mwalimu anayepaswa kumwondoa mwanafunzi mwenye ulemavu darasani hadi atakapothibitisha na Mwalimu Mkuu au Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu Maalum kuwa hatua ya kumwondoa mwanafunzi huyo darasani haitakiuka haki za mwanafunzi huyo chini ya sheria na kanuni za jimbo au za kitaifa.

6. **Kusimamishwa Shule**: Hatua za kusimamishwa shule zitachukuliwa tu kwa wanafunzi wanaosababisha hatari ya moja kwa moja au ambao ni hatari kwao binafsi au kwa wengine au ni wasumbufu zaidi au ambao, hatua za urekebishaji hazijafanya kazi.

Kusimamishwa shule ni hatua kali, inayoweza kuchukuliwa tu kwa wanafunzi ambao ni wakaidi zaidi, wasio watulivu, wenye vurugu au wasumbufu zaidi, au ambao tabia yao inahatarisha usalama, maadili, afya au ustawi wa wengine.

Hatua za kusimamishwa kwenda shule zitatumika kwa kiwango cha chini zaidi kinachohitajika ili kukuza na kuboresha tabia ya mwanafunzi na kuhakikisha mwanafunzi anahudhuria shule wakati wote.

Bodi ya Elimu ina mamlaka ya kuwasimamisha wanafunzi kwenda shuleni, lakini inaweka jukumu kuu la kuwasimamisha wanafunzi kwenda shuleni kwa Wasimamizi Wakuu na Wasimamizi wa Shule.

Mfanyakazi yeyote anaweza kumpendekezea Msimamizi Mkuu au Mwalimu Mkuu kuwa mwanafunzi fulani anapaswa kusimamishwa shule. Wafanyakazi wote lazima waripoti mara moja na waelekeze mwanafunzi mwenye vurugu kwa Mwalimu Mkuu au Msimamizi Mkuu kwa kuvunja kanuni za maadili mema. Mapendekezo na rufaa zote zinapaswa kuwasilishwa kwa maandishi isipokuwa hali za msingi za pendekezo au rufaa zinahitaji hatua kuchukuliwa mara moja. Katika hali hizo, ripoti ya maandishi inapaswa kutayarishwa haraka iwezekanavyo na mfanyakazi anayependekeza kuchukuliwa kwa hatua ya mwanafunzi kusimamishwa shule. Msimamizi Mkuu au Mwalimu Mkuu, baada ya kupokea pendekezo au rufaa ya kuchukuliwa kwa hatua ya mwanafunzi kusimamishwa shule au anaposhughulikia kesi ya mwanafunzi kusimamishwa shule, atakusanya maelezo yanayohusiana na suala hilo na kuyarekodi ili ayawasilishe baadaye, ikiwa inahitajika.

### A. Kusimamishwa Shule kwa Muda Mfupi (siku tano au chache)

Msimamizi Mkuu au Mwalimu Mkuu (anayerejelewa kama 'mwenye mamlaka ya kuwasimamisha wanafunzi shule') anapopendekeza kusimamishwa shule kwa mwanafunzi aliyeshtakiwa kwa tabia isiyofaa kwa siku tano au chache kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) kifungu cha §3214(3), mwenye mamlaka ya kuwasimamisha wanafunzi shule lazima amfahamishe mwanafunzi huyo mara moja kwa matamshi. Ikiwa mwanafunzi atakana kuhusiska na tabia hiyo isiyofaa mwenye mamlaka ya kuwasimamisha wanafunzi shule lazima aeleze msingi wa kuchukuliwa kwa hatua inayopendekezwa ya kusimamishwa shule. Mwenye mamlaka ya kuwasimamisha wanafunzi shule lazima pia afahamishe wazazi wa mwanafunzi kwa maandishi kuwa mwanafunzi anaweza kusimamishwa shule. Taarifa hiyo ya maandishi lazima iwasilishwe na mtu, au kwa njia nyingine iliyotathmini ipasavyo ili kuhakikisha taarifa hiyo inapokewa ndani ya saa 24 baada ya kufanya kwa uamuzi katika wiki ya kazi, wa kupendekeza kusimamishwa shule kwa anwani inayojulikana ya mzazi. Panapowezekana, taarifa hiyo inapaswa kuwasilishwa kwa simu ikiwa shule imepewa namba ya/za simu kwa makusudi ya kuwasiliana na wazazi.

Taarifa hiyo itatoa maelezo kuhusu mashtaka yaliyowasilishwa kumhusu mwanafunzi na tukio ambalo hatua ya kusimamishwa shule inapendekezwa kuchukuliwa na itawafahamisha wazazi kuhusu haki ya kuomba kufanya mkutano usio rasmi na Mwalimu Mkuu mara moja. Taarifa na mkutano usio rasmi vitatumia lugha au njia kuu ya mawasiliano inayotumika na wazazi. Katika mkutano huo, wazazi wataruhusiwa kuuliza maswali mashahidi wa mlalamikaji chini ya taratibu zitakazowekwa na Mwalimu Mkuu.

Taarifa na fursa ya kufanya mkutano usio rasmi vitafanyika kabla mwanafunzi hajasimamishwa shule isipokuwa iwapo uwepo wa mwanafunzi huyo shuleni unasababisha hatari kwa watu au mali au hatari ya kuvuruga utaratibu wa elimu. Ikiwa uwepo wa mwanafunzi huyo shuleni unasababisha hatari au usumbufu, taarifa na fursa ya kufanya mkutano usio rasmi vitafanyika mara tu baada ya mwanafunzi kusimamishwa shule kadri iwezekanavyo.

Baada ya mkutano huo, Mwalimu Mkuu atamfahamisha mzazi haraka iwezekanavyo kwa maandishi kuhusu uamuzi uliofanywa. Mwalimu Mkuu atamfahamisha mzazi kuwa ikiwa hajaridhika na uamuzi uliofanywa na angependa kufuatilia suala hilo zaidi, lazima akate rufaa kwa maandishi kwa Msimamizi Mkuu ndani ya siku kumi (10) za kazi, isipokuwa abainishe hali zisizo za kawaida zinazomzuia kufanya hivyo. Msimamizi Mkuu atatoa uamuzi kuhusu rufaa hiyo kwa maandishi ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya kupokea rufaa hiyo. Ikiwa wazazi hawajaridhishwa na uamuzi wa Msimamizi Mkuu, lazima wakate rufaa kwa maandishi kwa Bodi ya Elimu kupitia Karani wa Wilaya ndani ya siku kumi (10) za kazi kutoka tarehe ya kutolewa kwa uamuzi wa Msimamizi Mkuu, isipokuwa waweze kubainisha hali zisizo za kawaida zinazowazuia kufanya hivyo. Maamuzi ya mwisho pekee ya Bodi ya Elimu ndiyo yanaweza kukatiwa rufaa kwa Mkuu wa Elimu ndani ya siku thelathini (30) baada ya uamuzi kutolewa.

**B. Kusimamishwa Shule kwa Muda Mrefu (zaidi ya siku tano)**

Msimamizi Mkuu anapoamua kuwa hatua ya kusimamishwa shule kwa zaidi ya siku tano inaweza kufaa kuchukuliwa, lazima atoe taarifa mapema kwa mwanafunzi na wazazi wa mwanafunzi huyo kuhusu haki ya kukata rufaa. Katika kikao cha kesi, mwanafunzi atakuwa na haki ya kuwakilishwa na wakili, haki ya kuwauliza maswali mashahidi wa mlalamikaji na haki ya kuwasilisha mashahidi na ushahidi mwingine kwa niaba yake.

Msimamizi Mkuu atasikiliza mwenyewe kesi hiyo na kuiamua au anaweza, kwa hiari yake, kumteua mwamuzi wa kuendesha kesi hiyo. Mwamuzi huyo atapewa idhini ya kuapisha na kutoa amri za kufika mahakamani kuhusiana na kesi iliyowasilishwa kwake. Rekodi ya kesi hiyo itawekwa, lakini hakuna manukuu ya stenografia yatakayohitajika. Rekodi ya sauti itachukuliwa kuwa rekodi ya kuridhisha. Mwamuzi atabainisha ukweli na kutoa mapendekezo kuhusu hatua ya adhabu inayofaa kwa Msimamizi Mkuu. Ripoti ya mwamuzi itakuwa ya ushauri tu, na Msimamizi Mkuu anaweza kuikubali yote au sehemu yake.

Rufaa kuhusu uamuzi wa Msimamizi Mkuu inaweza kukatwa kwa Bodi, ambayo itafanya uamuzi wake kulingana tu na rekodi iliyopewa. Rufaa zote zinazokatwa kwa Bodi lazima ziwe kwa maandishi na ziwasilishwe kwa karani wa wilaya ndani ya siku thelathini (30) kutoka tarehe ya kutolewa kwa uamuzi wa Msimamizi Mkuu, isipokuwa wazazi waweze kubainisha hali zisizo za kawaida zinazowazuia kufanya hivyo. Bodi inaweza kukubali uamuzi wote au sehemu ya uamuzi wa Msimamizi Mkuu. Maamuzi ya mwisho ya Bodi ya Elimu yanaweza kukatiwa rufaa kwa Mkuu wa Elimu ndani ya siku thelathini (30) baada ya uamuzi kutolewa.

**C. Kusimamishwa Shule Kabisa**

Hatua ya kusimamishwa shule kabisa huchukuliwa tu kwa hali zisizo za kawaida kama vile ambapo tabia ya mwanafunzi inasababisha hatari kwa maisha kwa usalama na ustawi wa wanafunzi wengine, wafanyakazi wa shule au mtu mwingine yeyote aliye shuleni kisheria au anayehudhuria shughuli ya shule.

**D. Utaratibu wa Baada ya Kusimamishwa Shule**

Bodi inaweza kuamrisha mwanafunzi arudi shuleni mapema baada ya kusimamishwa shule mwanafunzi anapokubali kwa hiari yake kushiriki katika madarasa maalum au ya ushauri, kama vile udhibiti wa hasira au usuluhishaji wa mgogoro. Bodi inaweza kutoa fursa hii kwa hiari yake. Ikiwa na wakati mwanafunzi na/au mzazi/mlezi atakubali chaguo hili, sheria na masharti yataelezwa kwa maandishi. Hata hivyo, ikiwa mwanafunzi atavunja sheria na masharti yaliyokubaliwa ndani ya kipindi fulani cha muda, sehemu ya hatua ya kusimamishwa shule ambayo haijachukuliwa inaweza kuchukuliwa

**E. Muda wa Chini wa Kusimamishwa Shule**

1. Wanafunzi wanaomiliki au kuja shuleni na silaha fulani

Mwanafunzi yeyote, isipokuwa mwanafunzi mwenye ulemavu, anayepatikana na hatia ya kuja shuleni na bunduki, kisu, kilipuzi au bomu ya kulipuka moto au vifaa vingine hatari vinavyoweza kusababisha jeraha la mwili au kifo anaweza kuchukuliwa hatua ya kusimamishwa shule kwa angalau mwaka mmoja. Kabla ya kusimamishwa shule, mwanafunzi huyo atakuwa na fursa ya kesi yake kusikilizwa kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha §3214. Msimamizi Mkuu ana mamlaka ya kubadilisha hatua ya kusimamishwa shule kwa mwaka mmoja kulinga na kesi. Anapoamua iwapo atabadilisha hatua iliyochukuliwa, Msimamizi Mkuu anaweza kuzingatia yafuatayo:

a. Umri wa mwanafunzi.
b. Gredi ya mwanafunzi shuleni.
c. Rekodi ya awali ya nidhamu ya mwanafunzi.
d. Imani ya Msimamizi Mkuu kuwa aina nyingine za adhabu zinaweza kufaa zaidi.
e. Mchango kutoka kwa wazazi, walimu na/au watu wengine.
f. Hali nyingine za kupunguza ukali wa adhabu.

Mwanafunzi mwenye ulemavu anaweza kusimamishwa shule kulingana na mahitaji ya sheria ya jimbo na ya kitaifa.

2. Wanafunzi wanaofanya vitendo vya vurugu kando na kumiliki au kuja na silaha fulani shuleni.

Mwanafunzi yeyote, isipokuwa mwanafunzi mwenye ulemavu, anayepatikana na hatia ya kufanya kitendo cha vurugu, kando na kuja shuleni na bunduki, kisu, kilipuzi au bomu ya kulipuka moto au vifaa vingine hatari vinavyoweza kusababisha jeraha la mwili au kifo anaweza kuchukuliwa hatua ya kusimamishwa shule kwa angalau siku moja. Ikiwa hatua iliyopendekezwa kuchukuliwa ni angalau kusimamishwa shule kwa siku moja, mwanafunzi na mzazi/mlezi wa mwanafunzi huyo watapewa taarifa na fursa ya kufanya mkutano usio rasmi inayopewa wanafunzi wote wanaosimamishwa shule kwa muda mfupi. Ikiwa hatua iliyopendekezwa kuchukuliwa inazidi kusimamishwa shule kwa siku tano, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa taarifa na fursa ya kusikilizw akwa kesi yao inayopewa wanafunzi wote wanaosimamishwa shule kwa muda mrefu. Msimamizi Mkuu ana mamlaka ya kubadilisha hatua ya kusimamishwa shule kwa angalau siku moja kulinga na kesi. Anapoamua iwapo atabadilisha hatua iliyochukuliwa, Msimamizi Mkuu anaweza kuzingatia sababu kama za kubadilisha hatua ya kusimamishwa shule kwa mwaka mmoja kwa kupatikana na silaha.

3. Wanafunzi wanaovuruga zaidi utaratibu wa elimu mara kwa mara au wanaoathiri zaidi uwezo wa mwalimu wa kudhibiti darasa mara kwa mara.

Mwanafunzi yeyote, isipokuwa mwanafunzi mwenye ulemavu, ambaye anavuruga zaidi utaratibu wa elimu mara kwa mara au anayeathiri zaidi uwezo wa mwalimu wa kudhibiti darasa mara kwa mara atasimamishwa shule kwa angalau siku moja. Kwa makusudi ya kanuni hizi za maadili mema, maneno "anavuruga zaidi mara kwa mara" yanamaanisha kujihusisha na tabia inayosababisha mwanafunzi kuondolewa darasani na mwalimu/walimu kulingana na Sheria ya Elimu (Education Law) Kifungu cha § 3214 (3-a) na kanuni hizi mara nne au zaidi katika muhula mmoja, au mara tatu au zaidi katika mihula mitatu. Ikiwa hatua iliyopendekezwa kuchukuliwa ni angalau kusimamishwa shule kwa siku moja, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa taarifa na fursa ya kufanya mkutano usio rasmi inayopewa wanafunzi wote wanaosimamishwa shule kwa muda mfupi. Ikiwa hatua iliyopendekezwa kuchukuliwa inazidi kusimamishwa shule kwa siku tano, mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi huyo watapewa taarifa na fursa ya kusikilizw akwa kesi yao inayopewa wanafunzi wote wanaosimamishwa shule kwa muda mrefu. Msimamizi Mkuu ana mamlaka ya kubadilisha hatua ya kusimamishwa shule kwa angalau siku moja kulinga na kesi. Anapoamua iwapo atabadilisha hatua iliyochukuliwa, Msimamizi Mkuu anaweza kuzingatia sababu kama za kubadilisha hatua ya kusimamishwa shule kwa mwaka mmoja kwa kupatikana na silaha.

**F. Rufaa**

1. Ushauri: Washauri wa shuleni, watoa huduma za jamii au wanasaikolojia wa shule watashughulikia rufaa zote za wanafunzi wa kushauriwa.
2. Maombi ya PINS: Wilaya inaweza kuwasilisha ombi la PINS (Person In Need of Supervision (Mtu Anayehitaji Kusimamiwa)) katika Mahakama ya Familia kwa mwanafunzi yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18 anayeonyesha kuwa anahitaji usimamizi na matibabu kwa:
    a. Kuwa na mazoea ya kutoroka shule na kutohudhuria shule inavyohitajika na sehemu ya kwanza ya Kifungu cha 65 cha Sheria ya Elimu (Education Law).
    b. Kutoweza kudhibitiwa au kwa kuwa na mazoea ya kutotii na kuzidi udhibiti wa kisheria wa shule.
    c. Kushiriki katika ukahaba kwa kuvunja Sheria ya Adhabu (Penal Law) Kifungu cha §230.00 (kushiriki au kukubali au kujitolea kufanya ngono na mtu mwingine kwa malipo); au
    d. Kuonekana kuwa mwanafunzi aliyetumiwa vibaya kingono chini ya Sheria ya Huduma za Jamii (Social Services Law) Kifungu cha §447-a(1)(a), (c), au (d), lakini mwanafunzi huyo lazima akubali kuwasilisha ombi la PINS.



Kwa vipengele vya 'a' na 'b' hapo juu, inapowasilisha ombi, wilaya lazima ieleze juhudi za udhibiti ambazo imechukua au huduma zilizotolewa kwa mwanafunzi huyo, na misingi ya kuamua kuwa madai hayo hayawezi kusuluhishwa bila ombi hilo.

3. Watoto Wahalifu na Watoto Wakosaji: Kwa wanafunzi wanaopatikana na hatia ya kuja na labda silaha (ilivyoelezwa katika kifungu cha 18 cha USC §930(g)(2) au bunduki (ilivyoelezwa katika kifungu cha 18 cha USC §921), Msimamizi Mkuu anahitajika kuwasilisha maombi yafuatayo:

a. Kwa Mwanasheria wa Kaunti ili kuwasilisha kesi ya mtoto mhalifu katika Mahakama ya Familia: Wanafunzi wote wenye umri wa chini ya miaka 16, isipokuwa wanafunzi wenye umri wa miaka 14 au 15 wanaotimiza masharti ya hali ya mtoto mkosaji chini ya Sheria ya Utaratibu wa Uhalifu (Criminal Procedure Law) kifungu cha 1.20(42).

b. Kwa mamlaka zinazofaa za utekelezaji wa sheria: Wanafunzi wote wenye umri wa miaka 16, na wanafunzi wote wenye umri wa miaka 14 au 15 wanaotimiza masharti ya hali ya mtoto mkosaji chini ya Sheria ya Utaratibu wa Uhalifu (Criminal Procedure Law) kifungu cha 1.20(42).

## Adhabu ya Wanafunzi wenye Ulemavu

Kuelewa kuwa adhabu kama "tukio la mafunzo" ni muhimu kwa mbinu bora ya kuadhibu kwa lengo kuu la kufunza tabia njema ya kijamii. Kwa hivyo, bodi inaidhinisha mbinu za urekebishaji zitumike panapofaa. Mbinu hii inalenga uwajibikaji wa papo hapo na mabadiliko ya tabia.

Hatua za kuchukuliwa, na ikihitajika adhabu, husaidia zaidi vinaposhughulikia tatizo moja kwa moja wakati na mahali linapotokea, na kwa njia ambayo wanafunzi wanaona kuwa ni ya haki na isiyoegemea upande wowote. Wafanyakazi wa shule wanaoshirikiana na wanafunzi wanatarajiwa kutumia hatua ya adhabu panapohitajika tu na kusisitiza uwezo wa wanafunzi wa kukuza nidhamu yao.

Bodi pia inatambua kuwa wanafunzi wenye ulemavu wanaochukuliwa kuwa wanastahili kupokea huduma za elimu maalum chini ya sheria ya IDEA na Kifungu cha 89 cha Sheria ya Elimu ya New York wana haki fulani za ulinzi ambazo wasimamizi wa shule lazima wazingatie wanapoamua kuwasimamisha shule au kuwaondoa darasani. Chini ya hali fulani, haki hizo za ulinzi zinatumika pia kwa wanafunzi ambao kwa sasa hawachukuliwi kuwa mwanafunzi mwenye ulemavu lakini ambaye amebainishwa kuwa mwanafunzi anayedhaniwa kuwa na ulemavu kwa makusudi ya adhabu.

Kwa hivyo, Bodi imejitolea kuhakikisha kuwa wilaya inafuata taratibu za kusimamishwa shule na kuondolewa darasani zinazolingana na haki hizo za ulinzi. Kanuni za maadili mema za wanafunzi zinakusudiwa kuwapa wanafunzi wenye ulemavu na wanafunzi wanaodhaniwa kuwa na ulemavu, kwa makusudi ya adhabu, haki za moja kwa moja wanazofurahia chini ya sheria na kanuni zinazotumika.

**Ufafanuzi:** Kwa makusudi ya sehemu hii ya kanuni za maadili mema na kulingana na sheria na kanuni zinazotumika, ufafanuzi ufuatao utatumika:

1. "Mpango wa Msaada wa Kitabia" (Behavioral Intervention Plan, BIP) inamaanisha mpango unaotokana na matokeo ya utathmini wa tabia ya utendaji na ambao, angalau, unajumuisha maelezo ya tabia ya kutatiza, nadharia za jumla na maalum kuhusu kwa nini tabia hiyo ya kutatiza hutokea, na mikakati ya usaidizi inayojumuisha huduma na misaada inayofaa ya kitabia ya kushughulikia tabia hiyo.
2. "Dawa inayodhibitiwa" inamaanisha utumiaji mbaya wa dawa ya kulevya au dawa nyingine iliyotambuliwa chini ya ratiba ya I, II, III, IV au V katika kifungu cha 202(c) cha Sheria ya Vitu Vinavyodhibitiwa (Controlled Substances Act) (21 USC § 812(c)).
3. "Adhabu ya kubadilisha mpango" inamaanisha hatua ya kusimamishwa au kuondolewa kwa mwanafunzi kwenye mpango wake wa sasa wa elimu ambayo labda ni:
    a. Kwa zaidi ya siku kumi (10) mfululizo za shule; au
    b. Kwa kipindi cha siku kumi (10) mfululizo za shule au chache ikiwa mwanafunzi amekuwa na mfululizo wa matukio ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani ambayo yanaunda mtindo kwa sababu yanazidi jumla ya siku kumi (10) za shule katika mwaka wa shule, kwa sababu tabia ya mwanafunzi inafanana zaidi na tabia ya mwanafunzi katika matukio ya awali yaliyosababisha mfululizo wa matukio ya kuondolewa darasani, na kwa sababu ya vigezo vya ziada kama vile urefu wa muda wa kila tukio la kusimamishwa shule au kuondolewa darasani, jumla ya muda ambao mwanafunzi ameondolewa darasani na ukaribu wa matukio ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani.
4. "Dawa iliyopigwa marufuku" inamaanisha dawa inayodhibitiwa, lakini haijumuishi dawa inayodhibitiwa inayomilikiwa kisheria au inayotumika chini ya usimamizi wa mtaalamu wa huduma ya afya aliye na leseni, au dawa ambayo inamilikiwa kisheria au inayotumika kulingana na mamlaka ya Sheria ya Dawa Zinazodhibitiwa (Controlled Substances Act) au kulingana na kifungu kingine chochote cha sheria ya kitaifa.
5. "Mpango Tofauti wa Muda wa Elimu" (Interim Alternative Educational Setting, IAES) inamaanisha mpango wa muda wa elimu, kando na mpango wa sasa wa mwanafunzi wakati tabia iliyosababisha IAES ilitokea. Mpango wa IAES lazima uruhusu mwanafunzi kuendelea kupokea huduma za elimu zinazomwezesha kuendelea kushiriki katika mtaala wa jumla na kupiga hatua za kufanikisha malengo yaliyowekwa katika mpango binafsi wa elimu ya mwanafunzi; pamoja na kufanyiwa, ipasavyo, utathmini wa tabia ya utendaji na huduma za msaada wa kitabia na marekebisho yanayokusudiwa kushughulikia tabia isiyofaa ili isijirudie.
6. "Ukaguzi wa Uamuzi wa Tabia" (Manifestation Determination Review, MDR) inamaanisha ukaguzi wa uhusiano kati ya ulemavu wa mwanafunzi na tabia inayochukuliwa hatua ya adhabu inayohitajika wakati hatua ya adhabu inasababisha

adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu, na kufanyika kulingana na mahitaji yaliyoelezwa baadaye katika sera hii.

7. "Timu ya uamuzi wa tabia" inamaanisha mwakilishi wa wilaya anayemfahamu mwanafunzi na ufafanuzi wa maelezo kuhusu tabia ya mtoto, mzazi na washirika wanaohusika wa kamati kuhusu elimu maalum ilivyoamuliwa na mzazi na wilaya.

8. "Kuondolewa" inamaanisha kuondolewa kwa mwanafunzi mwenye ulemavu kwa sababu za adhabu kwenye mpango wake wa sasa wa elimu, kuliko kusimamishwa shule; na kubadilishwa kwa hatua ya kumweka mwanafunzi mwenye ulemavu kwenye mpango wa IAES.

9. "Siku ya shule" inamaanisha siku yoyote, ikijumuisha nusu siku, ambayo wanafunzi wako shuleni kwa makusudi ya mafunzo.

10. "Jeraha kubwa la mwili" inamaanisha jeraha la mwili linalohusisha hatari kubwa ya kusababisha kifo, maumivu makali ya mwili, jeraha la kudumu la kusababisha badiliko la wazi la sehemu ya mwili au jeraha la kudumu la kusababisha kushindwa au kasoro ya utendakazi wa sehemu ya mwili, kiungo au akili.

11. "Mwanafunzi anayedhaniwa kuwa na ulemavu kwa makusudi ya adhabu" inamaanisha mwanafunzi ambaye, chini ya hali zilizoelezwa baadaye kwenye sera hii, wilaya inachukuliwa kuwa ilikuwa na ufahamu kuwa alikuwa mwanafunzi mwenye ulemavu kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha kuchukuliwa hatua ya adhabu.

12. "Kusimamishwa shule" inamaanisha kusimamishwa shule kulingana na Kifungu cha §3214 cha Sheria ya Elimu ya New York.

13. "Silaha" ina maana sawa na neno "silaha hatari" kulingana na Kifungu cha 18 cha USC §930(g)(2) ambayo inajumuisha silaha, kifaa, chombo au kitu, chenye uhai au kisicho hai, kinachotumika au kinachoweza kusababisha kifo au jeraha kubwa la mwili.

"Silaha' pia inamaanisha bunduki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 18 cha USC §921 kwa makusudi ya Sheria ya Kukataza Bunduki Shuleni (Gun-Free Schools Act). Inamaanisha pia bunduki nyingine yoyote, bunduki ya BB, bastola, revolva, bunduki fupi, bunduki ndefu, bunduki ya mashine, mfano wa bunduki, daga, daga fupi, wembe, kisu chembamba kirefu, kisu cha kubadilisha makali, kisu cha kuchomoka, konzi za chuma, kombeo, kisu cha konzi ya chuma, vifaa vya kukatia boksi, upanga wa fimbo, bunduki ya kielektroniki ya kupooza mtu, nyota ya Kung Fu, bunduki ya kielektroniki ya kuduwaza mtu, kifaa cha kupuliza pilipili au kifaa kingine cha kupuliza kitu cha kudhuru, bomu ya kulipuka au ya moto, au kifaa, chombo au kitu kingine kinachoweza kusababisha jeraha la mwili au kifo kinapotumika kusababisha jeraha la mwili au kifo. Ingawa haijawekwa chini ya ufafanuzi wa silaha, utumiaji au umiliki wa nyembe zozote, vifaa vya kukatia baoksi, visu vya ukubwa wowote au kifaa kingine chochote kilicho na makali ya aina yoyote hairuhusiwi pia, isipokuwa iruhusiwe moja kwa moja na msimamizi. Ukipatikana na vitu vyovyote ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vitu hivi unaweza kuchukuliwa hatua ya adhabu.

**Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule ya Kuwasimamisha Shule au Kuwaondoa Darasani Wanafunzi wenye Ulemavu**

Bodi, Msimamizi Mkuu wa Wilaya, Msimamizi wa Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu mwenye mamlaka ya kuwasimamisha shule wanafunzi kulingana na Sheria ya Elimu anaweza kuamuru mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES, mpango mwingine au kusimamishwa shule kwa muda usiozidi siku tano (5) mfululizo za shule.

Msimamizi Mkuu anaweza, moja kwa moja au baada ya kupokea pendekezo la mwamuzi aliyeteuliwa, kuamrisha mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES, mpango mwingine au kusimamishwa shule kwa muda usiozidi siku kumi (10) mfululizo za shule ikijumuisha kipindi chochote ambacho mwanafunzi anasimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa tabia iyo hiyo kulingana na kifungu cha hapo juu, ikiwa Msimamizi Mkuu ataamua kuwa tabia ya mwanafunzi inasababisha kusimamishwa shule. Msimamizi Mkuu anaweza pia kuamrisha hatua zaidi za kusimamishwa shule kwa muda usiozidi siku kumi (10) mfululizo za shule katika mwaka mmoja wa shule kwa matukio tofauti ya utovu wa nidhamu, mradi hatua hizo za kusimamishwa shule hazisababishi adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu.

Kuongezea, Msimamizi Mkuu anaweza kuamrisha mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES, mpango mwingine au kusimamishwa shule kwa muda unaozidi siku kumi (10) mfululizo za shule ikiwa timu ya uamuzi wa tabia itaamua kuwa tabia ya mwanafunzi huyo haikutokana na ulemavu wa mwanafunzi huyo. Katika hali hiyo, Msimamizi Mkuu anaweza kumwadhibu mwanafunzi kwa njia sawa na kwa muda sawa kama mwanafunzi asiye mlemavu.

Zaidi ya hayo, Msimamizi Mkuu anaweza, moja kwa moja au baada ya kupokea pendekezo la mwamuzi aliyeteuliwa, kuamrisha mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES utakaoamuliwa na kamati kuhusu elimu maalum kwa muda wa hadi siku 45 za shule ikiwa mwanafunzi huyo labda:

1. Atapatikana au atakuja na silaha shuleni, kwenye majengo ya shule au katika shughuli ya shule, au "Silaha' pia inamaanisha bunduki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 18 cha USC §921 kwa makusudi ya Sheria ya Kukataza Bunduki Shuleni (Gun-Free Schools Act). Inamaanisha pia bunduki nyingine yoyote, bunduki ya BB, bastola, revolva, bunduki fupi, bunduki ndefu, bunduki ya mashine, mfano wa bunduki, daga, daga fupi, wembe, kisu chembamba kirefu, kisu cha kubadilisha makali, kisu cha kuchomoka, konzi za chuma, kombeo, kisu cha konzi ya chuma, vifaa vya kukatia boksi, upanga wa fimbo, bunduki ya kielektroniki ya kupooza mtu, nyota ya Kung Fu, bunduki ya kielektroniki ya kuduwaza mtu, kifaa cha kupuliza pilipili au kifaa kingine cha kupuliza kitu cha kudhuru, bomu ya kulipuka au ya moto, au kifaa, chombo au kitu kingine kinachoweza kusababisha jeraha la mwili au kifo kinapotumika kusababisha jeraha la mwili au kifo. Ingawa haijawekwa chini ya ufafanuzi wa silaha, utumiaji au umiliki wa nyembe zozote, vifaa vya kukatia baoksi, visu vya ukubwa wowote au kifaa kingine chochote kilicho na makali ya aina yoyote hairuhusiwi pia, isipokuwa iruhusiwe moja kwa moja na msimamizi. Ukipatikana na vitu vyovyote ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vitu hivi unaweza kuchukuliwa hatua ya adhabu.
2. Atapatikana au atatumia dawa zilizopigwa marufuku au atauza au ataomba kuuza dawa zinazodhibitiwa kimakusudi shuleni, kwenye majengo ya shule au katika shughuli ya shule ya chini ya mamlaka ya wilaya, au
3. Amesababisha jeraha kubwa la mwili kwa mtu mwingine akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule au katika shughuli ya shule ya chini ya mamlaka ya wilaya.

Msimamizi Mkuu anaweza kuamrisha mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES katika hali hizo, iwe tabia ya mwanafunzi huyo inatokana na ulemavu wa mwanafunzi huyo au la. Hata hivyo, kamati kuhusu elimu maalum itaamua mpango wa IAES.

**Taratibu za Wafanyakazi wa Shule za Kuwasimamisha Shule au Kuwaondoa Darasani Wanafunzi wenye Ulemavu**

1. Katika kesi zinazohusisha hatua ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa mwanafunzi mwenye ulemavu kwa muda wa siku tano (5) mfululizo za shule au chache, wazazi wa mwanafunzi huyo au watu wenye uhusiano wa uzazi na mwanafunzi huyo watafahamishwa kuhusu hatua hiyo ya kusimamishwa shule na kupewa fursa ya kufanya mkutano usio rasmi kulingana na taratibu sawa zinazotumika kwa hatua za kusimamishwa shule kwa muda mfupi kwa wanafunzi wasio walemavu.
2. Hatua ya kusimamishwa shule kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa muda unaozidi siku tano (5) za shule itafuata taratibu sawa za kisheria zinazotumika kwa wanafunzi wasio walemavu, isipokuwa iwapo kesi ya adhabu ya mwanafunzi itakayofanywa na Msimamizi Mkuu au mwamuzi aliyeteuliwa igawanywe katika awamu ya hatia na awamu ya adhabu. Baada ya kupatikana na hatia, Msimamizi Mkuu au mwamuzi aliyeteuliwa atasubiri taarifa ya uamuzi kutoka kwa timu ya uamuzi wa tabia iwapo tabia hiyo ya mwanafunzi ilitokana na ulemavu wake. Awamu ya adhabu ya kesi inaweza kuendelea baada ya kupokewa kwa taarifa hiyo. Ikiwa timu ya uamuzi wa tabia itaamua kuwa tabia hiyo haikutokana na ulemavu wa mwanafunzi, mwanafunzi huyo anaweza kuadhibiwa kwa njia sawa na mwanafunzi asiye mlemavu, isipokuwa kwamba ataendelea kupokea huduma zilizoelezwa hapa chini. Hata hivyo, ikiwa tabia hiyo itachukuliwa kuwa ilitokana na ulemavu wa mwanafunzi, kesi hiyo itafutwa, isipokuwa iwapo tabia husika ilihusiana na silaha, dawa zilizopigwa marufuku au dawa zinazodhibitiwa, au usababishaji wa jeraha kubwa la mwili, ambapo mwanafunzi huyo anaweza kuwekwa katika mpango wa IAES.

**Kikomo cha Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule ya Kuwasimamisha Shule au Kuwaondoa Darasani Wanafunzi wenye Ulemavu**

Kuchukuliwa kwa hatua ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani na mfanyakazi wa shule aliyeidhinishwa hakuwezi kusababisha adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu ya mwanafunzi mwenye ulemavu kutokana na mtindo wa matukio ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kama ilivyoelezwa hapo juu katika sehemu ya Ufafanuzi ya sera hii, isipokuwa:

1. Timu ya uamuzi wa tabia iamue kuwa tabia ya mwanafunzi haikutokana na ulemavu wake, au
2. Mwanafunzi aondolewe kwenye mpango wa IAES kwa sababu ya tabia inayohusiana na silaha, dawa zilizopigwa marufuku au dawa zinazodhibitiwa, au kwa kusababisha jeraha kubwa la mwili kama ilivyoelezwa hapo juu.

Wafanyakazi wa shule watazingatia hali zozote za kipekee kulingana na kesi wanapoamua iwapo adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu inafaa kwa mwanafunzi mwenye ulemavu anayevunja kanuni za maadili mema za wilaya.

Kuongezea, wafanyakazi wa shule hawapaswi kumsimamisha shule au kumwondoa darasani mwanafunzi mwenye ulemavu zaidi ya muda ambao mwanafunzi asiye mlemavu anaweza kusimamishwa shule kwa tabia kama hiyo.

**Taarifa kwa Mzazi Kuhusu Adhabu ya Kubadilishwa kwa Mpango wa Elimu:** Wilaya itawatumia wazazi wa mwanafunzi mwenye ulemavu taarifa kuhusu uamuzi wowote wa kuondolewa darasani unaosababisha adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu kwa sababu ya kuvunja kanuni za maadili mema ya mwanafunzi. Taarifa hiyo itaambatana na nakala ya taarifa ya haki za ulinzi.

**Mamlaka ya Mwamuzi Asiyeegemea Upande Wowote ya Kumwondoa Darasani Mwanafunzi mwenye Ulemavu**: Mwamuzi asiyeegemea upande wowote anaweza kuamrisha mwanafunzi mwenye ulemavu awekwe katika mpango wa IAES kwa muda wa hadi siku 45 za shule kwa wakati mmoja ikiwa ataamua kuwa kumwacha mwanafunzi kwenye mpango wake wa sasa wa elimu kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mwanafunzi au kwa wengine. Mamlaka haya yanatumika iwe tabia ya mwanafunzi inatokana na ulemavu wake au la.

**Ukaguzi wa Uamuzi wa Tabia:** Timu ya uamuzi wa tabia, ikiwezekana, itafanya mara moja ukaguzi wa uhusiano kati ya ulemavu wa mwanafunzi na tabia inayosababisha kuchukuliwa kwa hatua ya adhabu ili kutambua ikiwa tabia hiyo inatokana na ulemavu wa mwanafunzi, lakini haipaswi kuwa baada ya siku 10 za shule baada ya uamuzi kufanywa na:

1. Msimamizi Mkuu wa kubadilisha mpango wa elimu ya mwanafunzi kuwa IAES;
2. Mwamuzi asiyeegemea upande wowote wa kumweka mwanafunzi katika mpango wa IAES; au
3. Bodi, Msimamizi Mkuu au Mwalimu Mkuu wa Shule kuchukua hatua ya kumsimamisha shule mwanafunzi inayosababisha adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu.

Timu ya uamuzi wa tabia lazima iamue kuwa tabia ya mwanafunzi ilitokana na ulemavu wake ikiwa itaamua kuwa tabia husika labda:

1. Ilisababishwa au ilikuwa na uhusiano mkubwa wa moja kwa moja na ulemavu wa mwanafunzi, au
2. Ilisababishwa moja kwa moja na hatua ya wilaya ya kushindwa kutekeleza mpango binafsi wa elimu ya mwanafunzi.

Uamuzi wa timu ya uamuzi wa tabia lazima utokane na ukaguzi wa maelezo yote yanayohusika yaliyo kwenye faili ya mwanafunzi ikijumuisha mpango binafsi wa elimu ya mwanafunzi, uchunguzi wowote wa mwalimu na maelezo yoyote yanayohusika yaliyotolewa

na wazazi.

Ikiwa timu ya uamuzi wa tabia itaamua kuwa tabia ya mwanafunzi inatokana na ulemavu wake, wilaya:

1. Itaitaka kamati kuhusu elimu maalum ifanye utathmini wa tabia ya utendaji ya mwanafunzi na kutekeleza mpango wa msaada wa kitabia, isipokuwa wilaya iwe tayari imefanya hivyo kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu. Hata hivyo, ikiwa mwanafunzi tayari ana mpango wa msaada wa kitabia, CSE itakagua mpango huo na jinsi unavyotekelezwa na kuurekebisha inavyohitajika ili ushughulikie tabia hiyo.
2. Itamrejesha mwanafunzi kwenye mpango wa elimu alioondolewa, isipokuwa iwapo mpango wa elimu ulibadilishwa kuwa IAES kwa sababu ya tabia inayohusiana na silaha, dawa zilizopigwa marufuku au dawa zinazodhibitiwa au kwa kusababisha jeraha kubwa la mwili, au iwapo wazazi na wilaya wanakubali kubadilishwa kwa mpango wa elimu kama sehemu ya urekebishaji wa mpango wa msaada wa kitabia.

Ikiwa timu ya uamuzi wa tabia itaamua kuwa tabia husika ilitokana moja kwa moja na hatua ya wilaya ya kushindwa kutekeleza mpango binafsi wa elimu ya mwanafunzi, wilaya itachukua hatua mara moja ili kurekebisha mapungufu hayo.

**Huduma kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wakati wa Vipindi vya Kusimamishwa Shule au Kuondolewa Darasani**

Wanafunzi wenye ulemavu waliosimamishwa shule au walioondolewa kwenye mpango wao wa sasa wa elimu kulingana na kanuni za sera hii na kanuni na sheria zinazotumika wataendelea kupokea huduma ifuatavyo:

1. Katika matukio ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa muda wa hadi siku kumi (10) za shule katika mwaka wa shule ambayo hayasababishi adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu, wilaya itatoa mpango mwingine wa mafunzo kwa wanafunzi wenye ulemavu wenye umri wa kuhudhuria kwa lazima kwa msingi sawa kama wanafunzi wasio walemavu. Wanafunzi wenye ulemavu ambao hawajafikisha umri wa kuhudhuria kwa lazima watapokea huduma katika vipindi hivyo vya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa kiwango sawa na wanafunzi wasio walemavu wenye umri kama wao waliosimamishwa shule.
2. Katika matukio yanayofuata ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa muda wa hadi siku kumi (10) za shule ambayo kwa ujumla yanazidi siku kumi (10) za shule katika mwaka wa shule lakini hayasababishi adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu, wilaya itawapa wanafunzi wenye ulemavu huduma zinazohitajika ili kuwawezesha kuendelea kushiriki katika mtaala wa jumla wa elimu na kupiga hatua za kufanikisha malengo yaliyowekwa kwenye mipango yao binafsi ya elimu. Wafanyakazi wa shule, kwa kushauriana na angalau mmoja wa walimu wa mwanafunzi, wataamua kiwango cha huduma zinazohitajika ili kutii mahitaji haya. Kuongezea, katika vipindi hivyo vya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani, wilaya itawapa pia wanafunzi wenye ulemavu huduma wanazohitaji kupokea, ipasavyo, kuwafanyia utathmini wa tabia ya utendaji na huduma za msaada wa kitabia na marekebisho yanayokusudiwa kushughulikia tabia isiyofaa ili isijirudie.
3. Katika matukio ya kusimamishwa shule au kuondolewa darasani kwa zaidi ya siku kumi (10) za shule katika mwaka wa shule, yanayosababisha adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu, ikijumuisha kuwekwa katika mpango wa IAES kwa sababu ya tabia inayohusiana na silaha, dawa zilizopigwa marufuku au dawa zinazodhibitiwa, au kwa kusababisha jeraha kubwa la mwili, wilaya itawapa wanafunzi wenye ulemavu huduma zinazohitajika ili kuwawezesha kuendelea kushiriki katika mtaala wa jumla, kupiga hatua za kufanikisha malengo yaliyowekwa kwenye mipango yao binafsi ya elimu, na kufanyiwa utathmini wa tabia ya utendaji, ipasavyo, na huduma za msaada wa kitabia na marekebisho yanayokusudiwa kushghulikia tabia isiyofaa ili isijirudie.

Katika tukio kama hilo, kamati kuhusu elimu maalum itaamua huduma zinazofaa kutolewa.




**Wanafunzi Wanaodhaniwa Kuwa na Ulemavu kwa Makusudi ya Adhabu**

Mzazi wa mwanafunzi anayechukuliwa hatua ya adhabu lakini ambaye hakutambulishwa kama mwanafunzi mwenye ulemavu wakati tukio la tabia isiyofaa lilipotokea ana haki ya kutumia haki zozote za ulinzi zilizoelezwa kwenye sera hii kulingana na kanuni na sheria zinazotumika, ikiwa wilaya itachukuliwa kuwa ilikuwa na ufahamu kuwa mwanafunzi huyo alikuwa ni mwanafunzi mwenye ulemavu kabla ya kutokea kwa tukio la tabia inayosababisha kuchukuliwa hatua ya adhabu kwa hivyo mwanafunzi huyo atadhaniwa kuwa ana ulemavu kwa makusudi ya adhabu.

Ikiwa itadaiwa kuwa wilaya ilikuwa na ufahamu huo, litakuwa jukumu la Msimamizi Mkuu, Mwalimu Mkuu wa Shule au afisa mwingine wa shule aliyeidhinishwa kuchukua hatua husika ya kumsimamisha shule au kumwondoa mwanafunzi darasani kuamua iwapo mwanafunzi huyo ni mwanafunzi anayedhaniwa kuwa na ulemavu kwa makusudi ya adhabu. Wilaya itachukuliwa kuwa ilikuwa na ufahamu huo ikiwa:

1. Mzazi wa mwanafunzi aliripoti wasiwasi wake kwa maandishi kwa mfanyakazi wa uangalizi au usimamizi, au kwa mwalimu wa mwanafunzi kuwa mwanafunzi huyo anahitaji elimu maalum. Ripoti hiyo inaweza kuwa kwa matamshi ikiwa mzazi hajui kuandika au ana ulemavu unaomzuia kuwasilisha taarifa ya maandishi; au
2. Mzazi wa mwanafunzi ameomba mwanafunzi huyo afanyiwe utathmini; au
3. Mwalimu wa mwanafunzi huyo au mfanyakazi mwingine wa shule ameripoti wasiwasi fulani kuhusu mtindo wa tabia inayoonyeshwa na mwanafunzi huyo, moja kwa moja kwa mkurugenzi wa elimu maalum wa wilaya au mfanyakazi mwingine wa usimamizi.

Isitoshe, mwanafunzi hatachukuliwa kuwa mwanafunzi anayedhaniwa kuwa na ulemavu kwa makusudi ya adhabu ikiwa licha ya wilaya kupokea maelezo yanayothibitisha dai kuwa ilikuwa na ufahamu kuwa mwanafunzi huyo ana ulemavu,

1. Mzazi wa mwanafunzi hajaruhusu mwanafunzi huyo afanyiwe utathmini; au
2. Mzazi wa mwanafunzi amekataa huduma; au
3. Wilaya ilimfanyia mwanafunzi huyo utathmini na kutambua kuwa mwanafunzi huyo si mwanafunzi mwenye ulemavu. Ikiwa hakuna msingi wa kuthibitisha kuwa mwanafunzi huyo ni mwanafunzi mwenye ulemavu kabla ya mwanafunzi huyo kuchukuliwa hatua za adhabu, mwanafunzi huyo anaweza kuchukuliwa hatua sawa za adhabu kama mwanafunzi mwingine yeyote asiye mlemavu aliyehusika katia tabia kama hiyo. Hata hivyo, ikiwa wilaya itapokea ombi la kufanyiwa utathmini binafsi mwanafunzi akiwa amechukuliwa hatua ya adhabu ya kuondolewa darasani, wilaya itamfanyia mwanafunzi huyo utathmini wa haraka kulingana na sheria na kanuni zinazotumika. Hadi wakati ambapo utathmini wa haraka utakapofanywa, mwanafunzi atabaki kwenye mpango wa elimu ulioamuliwa na wilaya inayoweza kujumuisha kusimamishwa shule.

**Kesi za Kuamuliwa Haraka**

Wilaya itapanga kesi ya kuamuliwa haraka baada ya kupokea au kuwasilishwa kwa taarifa ya malalamiko ya kisheria ya kesi hiyo na:

1. Wilaya ili kupata amri ya mwamuzi asiyeegemea upande wowote ya kumweka mwanafunzi mwenye ulemavu katika mpango wa IAES pale ambapo mfanyakazi wa shule anasisitiza kuwa ni hatari kwa mwanafunzi huyo kuwa kwenye mpango wake wa sasa wa elimu;
2. Wilaya wakati wa kusubiri kuamuliwa kwa kesi pale ambapo mfanyakazi wa shule anasisitiza kuwa ni hatari kwa mwanafunzi huyo kuwa katika mpango wake wa sasa wa elimu wakati wa kusikilizwa kwa kesi hiyo;
3. Mzazi wa mwanafunzi kuhusiana na uamuazi kwamba tabia ya mwanafunzi haikutokana na ulemavu wake; au
4. Mzazi wa mwanafunzi kuhusiana na uamuzi wowote kuhusu mpango wa elimu, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu uamuzi wowote wa kumweka mwanafunzi katika mpango wa IAES.

Wilaya itapanga, na mwamuzi asiyeegemea upande wowote ataendesha kesi ya kusikilizwa haraka kulingana na taratibu zilizowekwa katika kanuni za Mkuu/Kamishna. Taratibu hizo ni pamoja na, lakini si tu kuandaa mkutano wa kutafuta suluhu, na kuanzisha na kukamilisha kesi ndani ya muda uliowekwa katika kanuni hizo.

Wakati kesi ya kuamuliwa haraka imeombwa kwa sababu ya adhabu ya kubadilishwa kwa mpango wa elimu, uamuzi wa tabia, au kwa sababu wilaya inaamini kuwa mwanafunzi akiendelea kuwa katika mpango wake wa sasa elimu inaweza kusababisha jeraha kwa mwanafunzi au wengine, mwanafunzi atabaki kwenye mpango wa IAES uamuzi wa mwamuzi asiyeegemea upande wowote unaposubiriwa au hadi kipindi cha kuondolewa kwenye mpango kitakapoisha, lolote litakalotangulia isipokuwa mzazi wa mwanafunzi na wilaya wakubali vinginevyo.

**Kuripotiwa kwa Mamlaka za Utekelezaji wa Sheria na Mahakamani**

Kulingana na mamlaka yake chini ya sheria na kanuni zinazotumika, wilaya itaripoti kosa linalofanywa na mwanafunzi mwenye ulemavu kwa mamlaka za utekelezaji wa sheria zinazofaa na mahakamani. Katika tukio kama hilo, Msimamizi Mkuu atahakikisha kuwa nakala za rekodi za adhabu na elimu maalum za mwanafunzi huyo zimetumwa ili zizingatiwe kwa mamlaka zinazofaa ambapo kosa hilo limeripotiwa, kadri ambavyo utumaji huo unaruhusiwa na Sheria ya Haki na Faragha ya Elimu ya Familia (Family Educational Rights and Privacy Act, FERPA).

## Mpango Mwingine wa Mafunzo

Mpango Mwingine wa Mafunzo unapaswa kulingana na sera ya mpango wa mafunzo ya nyumbani. Wanafunzi ambao wamesimamishwa shule watapewa mpango mwingine wa mafunzo. Mafunzo hayo yanaweza kutolewa nyumbani kwa mwanafunzi au mahali pengine, ikijumuisha mtandaoni, itakavyoamuliwa na wilaya, kwa kusawazisha maslahi bora ya mwanafunzi, usalama wa mfanyakazi wa wilaya na rasilimali za wilaya. Walimu wa mafunzo ya nyumbani wa wilaya wanaweza kutumika, ikiwa wapo. Mafunzo hayo hayadhibitiwi na masharti ya kanuni za jimbo kuhusu mafunzo ya nyumbani (8 NYCRR §100.22). Hata hivyo, wanafunzi waliofikisha umri wa lazima kwenda shule, lazima wapokee mafunzo kwa idadi sawa ya chini ya saa zinazohitajika kwa mafunzo ya nyumbani. Mafunzo hayo yoyote yatalingana zaidi na mafunzo ambayo mwanafunzi angepokea katika mazingira ya kawaida ya elimu, yatakayoamuliwa na wilaya kulingana na kesi.

## Upekuzi na Kumhoji Mwanafunzi

Bodi ya Elimu imejitolea kuhakikisha mazingira salama na yenye utulivu shuleni na katika shughuli za shule. Ili kuwezesha mazingira ya aina hii, afisa yeyote wa shule aliyeidhinishwa kumchukulia mwanafunzi hatua ya adhabu anaweza kumhoji mwanafunzi kuhusu tukio linalodaiwa la uvunjaji wa sheria au kanuni za maadili mema za wilaya. Wanafunzi hawana haki ya kupewa aina yoyote ya onyo la "Miranda" kabla ya kuhojiwa na maafisa wa shule, wala maafisa wa shule hawahitajiki kuwasiliana na mzazi/wazazi wa mwanafunzi kabla ya kumhoji mwanafunzi. Hata hivyo, maafisa wa shule watawaambia wanafunzi wote sababu ya kuhojiwa kwao.

Bodi inampa idhini Msimamizi Mkuu wa Shule, Walimu Wakuu wa Shule, muuguzi wa shule na maafisa wa ulinzi wa wilaya kuwapekua wanafunzi na vitu vyao, mara nyingi, kulingana na vizuizi vilivyowekwa katika kifungu cha A, B na C, (hapa chini), ikiwa afisa wa shule aliyeidhinishwa ana sababu nzuri ya kuamini kuwa upekuzi huo utasababisha kupatikana kwa ushahidi wa kuthibitisha kuwa mwanafunzi alivunja sheria au kanuni za maadili mema za wilaya.

Afisa wa shule aliyeidhinishwa anaweza kupekua vitu vya mwanafunzi kwa njia isiyo ya undani zaidi, kama vile kugusa sehemu ya nje ya begi ya vitabu, mradi afisa huyo wa shule ana sababu nzuri ya kufanya upekuzi huo mdogo.

Afisa wa shule aliyeidhinishwa anaweza kumpekua mwanafunzi au vitu vya mwanafunzi kulingana na habari alizopokea kutoka kwa mtoa habari wa kutegemewa. Watu binafsi, wasio wafanyakazi wa wilaya, watachukuliwa kuwa watoa habari wa kutegemewa ikiwa awali wamewahi kutoa habari zilizokuwa sahihi na zilizothibitishwa, au wanatoa habari kwa kutojali maslahi yao binafsi, au wanatoa habari sawa na zinazopokewa kutoka kwa vyanzo vingine huru, au wanaonekana kuwa wa kuaminika na habari wanazotoa zinahusiana na hatari ya moja kwa moja kwa usalama. Wafanyakazi wa wilaya watachukuliwa kuwa watoa habari wa kutegemewa isipokuwa wajulikane kuwa awali wamewahi kutoa habari ambazo walijua kuwa si sahihi.

Kabla ya kumpekua mwanafunzi au vitu vya mwanafunzi, afisa wa shule aliyeidhinishwa anapaswa kujaribu kumfanya mwanafunzi akubali kuwa ana ushahidi wazi kuwa alivunja sheria au kanuni za wilaya, au kmfanya mwanafunzi akubali kupekuliwa kwa hiari yake. Upekuzi hautazidi vikomo vilivyowekwa hapa chini ili kupata ushahidi unaotafutwa.

Panapowezekana, shughuli za upekuzi zitafanyiwa ndani ya afisi za usimamizi. Shughuli zote za upekuzi zitafanywa na msimamizi au mwakilishi wake na shahidi aliye mtu mzima, na wanafunzi watakuwepo wakati vitu vyao vinapekuliwa.

A. Makabati ya Wanafunzi, Madawati na Maeneo Mengine ya Hifadhi ya Shule

Kanuni zilizo kwenye kanuni hizi za maadili mema kuhusu upekuzi wa wanafunzi na vitu vyao hazitumiki kwa upekuzi wa makabati ya wanafunzi, madawati na maeneo mengine ya hifadhi ya shule. Wanafunzi hawatarajii usiri wowote kudumishwa kuhusiana na maeneo haya na maafisa wa shule wana udhibiti kamili kuhusu maeneo haya. Hii inamaanisha kuwa makabati ya wanafunzi, madawati na maeneo mengine ya hifadhi ya shule yanaweza kupekuliwa wakati wowote na maafisa wa shule, bila kutoa taarifa mapema kwa wanafunzi na bila idhini yao.

B. Upekuzi wa Mwili

Upekuzi wa kuvua nguo ni upekuzi unaohitaji mwanafunzi kuvua nguo yoyote au zote, isipokuwa koti au jaketi ya nje. Bodi ya Elimu inakataza kufanywa kwa upekuzi wa kuvua nguo. Afisa wa shule aliyeidhinishwa anaweza kufanya upekuzi wa mwili na kumtaka mwanafunzi avue koti au jaketi yake ya nje, iwapo kuna sababu nzuri ya kuamini kuwa mwanafunzi anaficha ushahidi wa kuvunja sheria au kanuni za maadili mema za wilaya.

C. Rekodi za Upekuzi

Afisa wa shule aliyeidhinishwa anayefanya upekuzi anawajibika kwa kurekodi haraka iwezekanavyo maelezo yafuatayo kuhusu kila shughuli ya upekuzi:

1. Jina, umri na gredi ya mwanafunzi aliyepekuliwa.
2. Sababu za upekuzi.
3. Jina la mtoa habari/watoa habari wowote.
4. Kusudi la upekuzi (yaani, kitu/vitu vilivyokuwa vinatafutwa).
5. Aina na kikomo cha upekuzi.
6. Mtu aliyefanya upekuzi na cheo na nafasi yake.
7. Walioshuhudia upekuzi huo.
8. Saa na mahali ambapo upekuzi ulifanywa
9. Matokeo ya upekuzi (yaani, kitu/vitu vilivyopatikana).
10. Utupaji wa vitu vilivyopatikana.
11. Saa, njia na matokeo ya mawasiliano na mzazi/mlezi.

Mwalimu Mkuu au mwakilishi wa Mwalimu Mkuu atawajibika kwa uzuiliaji, udhibiti na utupaji wa kitu chochote hatari au kilichopigwa marufuku kilichochukuliwa kutoka kwa mwanafunzi. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima aweke lebo wazi kwenye kila kitu kilichochukuliwa kutoka kwa mwanafunzi na aendelee kuzuilia kitu/viti hivyo, hadi kitu hicho kitakapokabidhiwa kwa polisi. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake anawajibika kwa kuwasilisha mwenyewe vitu hatari au vilivopigwa marufuku kwa polisi.

D. Kuhusisha Polisi katika Shughuli za Upekuzi na Kuwahoji Wanafunzi



Maafisa wa wilaya wamejitolea kushirikiana na maafisa wa polisi na mamlaka nyingine za utekelezaji wa sheria kudumisha mazingira salama ya shule. Maafisa wa polisi, hata hivyo, wana mamlaka madogo ya kuwahoji au kuwapekua wanafunzi shuleni au katika shughuli za shule, au kutumia majengo ya shule kuhusiana na kazi ya polisi. Maafisa wa polisi wanaweza kuingia shuleni au katika shughuli ya shule ili kumhoji au kumpekua mwanafunzi au kufanya uchunguzi rasmi unaohusisha wanafunzi ikiwa tu wana:

1. Kibali cha kufanya upekuzi au kukamata; au
2. Sababu nzuri ya kuamini kuwa tukio la uhalifu limefanyika shuleni au katika shughuli ya shule.
3. Wamekaribishwa na maafisa wa shule.

Kabla maafisa wa polisi hawajaruhusiwa kumhoji au kumpekua mwanafunzi, Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake lazima kwanza ajaribu kumfahamisha mzazi/mlezi wa mwanafunzi ili kumpa mzazi fursa ya kuwepo wakati wa kuhojiwa au kupekuliwa na polisi. Ikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi hapatikani kabla ya kuhojiwa au kupekuliwa na polisi, shughuli ya kuhojiwa au kupekuliwa na polisi haitafanyika. Mwalimu Mkuu au mwakilishi wake atakuwepo pia katika shughuli yoyote ya mwanafunzi kuhojiwa au kupekuliwa na polisi shuleni au katika shughuli ya shule.

Wanafunzi wanaohojiwa na maafisa wa polisi shuleni au katika shughuli ya shule watakuwa na haki sawa walizo nazo nje ya shule. Hii inamaanisha:

1. Lazima wafahamishwe kuhusu haki zao za kisheria.
2. Wanaweza kubaki kimya wakitaka.
3. Wanaweza kuomba kuwepo kwa wakili.

E. Ushughulikiaji wa Simu za Mkononi

Walimu na wasimamizi wana idhini ya kuchukua simu za mkononi za wanafunzi zinazotumika kinyume cha kanuni za maadili mema na/au Sera ya 5315 Vifaa vya Kielektroniki (Electronic Devices). Walimu na wasimamizi wanaruhusiwa kuangalia skrini ya simu ya mkononi na wanaweza kuomba mwanafunzi ashirikiane nao katika kupekua simu ya mkononi zaidi. Bila ruhusa ya mwanafunzi, walimu na wasimamizi hawapaswi kufanya upekuzi wa ndani zaidi hadi wapate ushauri kutoka kwa Msimamizi Mkuu au wakili wa shule.

## Adhabu ya Kuchapwa

Adhabu ya kuchapwa ni kitendo chochote cha kutumia nguvu kwa mwanafunzi kwa makusudi ya kumwadhibu mwanafunzi huyo. Adhabu ya kuchapwa kwa mwanafunzi yeyote na mfanyakazi yeyote wa wilaya hairuhusiwi kabisa.

Adhabu ya kuchapwa haijumuishi kutumia nguvu kumlinda mwanafunzi, mwanafunzi mwingine, mwalimu au mtu mwingine yeyote kutokana na kujeruhiwa kimwili, wakati taratibu na njia zingine zisizohusisha kutumia nguvu hazifai kutumika kufanikisha makusudi haya.

Hatua ya kutumia nguvu haitatumika kuzuia uharibifu wa mali, isipokuwa katika hali ambapo kuna hatari ya moja kwa moja ya kusababisha madhara makubwa kwa mwanafunzi au wengine, na mwanafunzi hajakubali kutumika kwa mikakati ya msaada mzuri wa haraka.

Matumizi yaliyoidhinishwa ya mapumziko na kutumia nguvu yameelezwa katika sera ya 4321.12.(hatuna sera ya 4321.12-R)

Wilaya itawasilisha malalamiko yote kuhusu matumizi ya adhabu ya kuchapwa kwa Mkuu/Kamishna wa Elimu kulingana na kanuni za Mkuu/Kamishna.

# Usambazaji na Ukaguzi

**A. Usambazaji wa Kanuni za Maadili mema**

Bodi itajitahidi kuhakikisha kuwa jamii inafahamu kanuni hizi za maadili mema kwa:

1. Kutoa nakala za muhtasari wa kanuni hizi kwa lugha rahisi kulingana na umri kwa wanafunzi wote katika mkutano utakaofanyika mwanzoni mwa kila mwaka wa shule.
2. Kutoa muhtasari wa lugha rahisi kwa mzazi/wazazi wote mwanzoni mwa mwaka wa shule na baadaye kwa kuombwa.
3. Kuchapisha kanuni kamili za maadili mema kwenye tovuti ya wilaya.
4. Kuwapa walimu wote wa sasa na wafanyakazi wengine nakala ya kanuni hizi na nakala ya marekebisho yoyote yakayofanywa kwenye kanuni hizi haraka iwezekanavyo baada ya kupitishwa.
5. Kuwapa wafanyakazi wote wapya nakala ya kanuni za maadili mema zinazotumika mara tu wanapoajiriwa.
6. Kufanya nakala za kanuni kamili zipatikane ili zisomwe na wanafunzi, mzazi/wazazi na wanajamii wengine T

Bodi itafadhili mpango wa elimu ya ndani huduma kwa wafanyakazi wote wa wilaya ili kuhakikisha utekelezaji bora wa kanuni za maadili mema na mafunzo mengine ya kuchangia katika ufanisi wake inavyohitajika. Msimamizi Mkuu anaweza kuomba mapendekezo ya wafanyakazi wa wilaya, hasa walimu na wasimamizi, kuhusu mipango ya ndani ya huduma kuhusiana na usimamizi na nidhamu ya wanafunzi. Maendeleo ya kitaalamu yatajumuishwa katika mpango wa wilaya wa maendeleo ya kitaalamu, inavyohitajika.

**B. Ukaguzi wa Kanuni za Maadili Mema**

Bodi itakagua kanuni hizi za maadili mema kila mwaka na kuzisahihisha inavyohitajika. Katika kufanya ukaguzi, Bodi itazingatia jinsi ambavyo vifungu vya kanuni vimefanya kazi na iwapo kanuni hizo zimetumika kwa haki na kwa uthabiti.

Kabla ya kupitisha marekebisho yoyote ya kanuni, Bodi itaandaa angalau kikao kimoja cha umma ambapo wafanyakazi wa shule, mzazi/wazazi, wanafunzi na mtu mwingine yeyote anayevutiwa wanaweza kushiriki.

Kanuni za maadili mema na marekebisho yoyote yanayofanywa vitawasilishwa kwa Mkuu/Kamishna wa Elimu, kwa njia iliyowekwa na Mkuu/Kamishna, kabla ya siku 30 kuisha baada ya kupitishwa.



# Kiambatisho cha A: Kamusi ya Maneno

Kwa makusudi ya Kanuni za Maadili Mema, ufafanuzi ufuatao unatumika.

**“Tabia”** ni njia ambayo mtu anatenda au kujionyesha, hasa kwa wengine. Inatarajiwa kuwa wanafunzi, wafanyakazi na wageni watajionyesha kwa njia inayolingana na Kanuni hizi za Maadili Mema.

“**Mwanafunzi msumbufu**’ inamaanisha mwanafunzi wa shule ya msingi au ya sekondari mwenye umri wa chini ya miaka 21 ambaye anavuruga zaidi utaratibu wa elimu au anayeathiri zaidi uwezo wa mwalimu wa kudhibiti darasa.

**“Jinsia”** inamaanisha jinsia ya kweli au inayodhaniwa na inajumuisha utambulisho au mwonekano wa kijinsia wa mtu.

**“Mwonekano wa kijinsia”** ni jinsi ambavyo mtu anaelezea au anaonyesha jinsia yake kwa wengine, mara nyingi kupitia tabia, mtindo wa nywele, shughuli, sauti au mienendo.

**“Utambulisho wa kijinsia”** ni jinsi mtu anavyojidhania kuwa mwanamume au mwanamke, tofauti na jinsia ya kweli ya kibiolojia au jinsia aliyopewa alipozaliwa.

**“Mzazi”** inamaanisha mzazi, mlezi au mtu mwenye uhusiano wa uzazi na mwanafunzi.

**“Mitindo ya nywele ya kujilinda”** ni pamoja na, lakini si tu mitindo ya nywele kama vile misuko, misokoto na mikunjo.

**“Asili”** inajumuisha sifa za kihistoria zinazohusishwa na asili, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, hali ya nywele na mitindo ya nywele ya kujilinda.

**“Mahusiano”** ni njia ambayo watu wawili au zaidi wanaheshimiana na kutendeana.

**“Heshima”** ni kitendo cha kuheshimu kila mtu katika jamii ya shule. Hii huonyeshwa kwa: kuwa mkarimu na mwenye kuwajali wengine, kuwa mpole na mwenye adabu, kueleza mawazo na dhana kwa njia za upole na adabu, kutumia lugha ya mwili na sauti ya upole, kuwasikiliza wengine wanaokuzungumzia, kukaa kwa utulivu na kutoingilia nafasi binafsi za wengine.

**“Uwajibikaji”** ni wajibu wa kutenda kulingana na kanuni za jamii na kuwajibishwa kwa vitendo vyako.

**“Hatua za Urekebishaji”** Hatua za urekebishaji zinatokana na hatua za kawaida zinazonyesha utu wetu wa jumla. Zikitumika ipasavyo, hujenga utamaduni wa kuvutia. Hatua za urekebishaji zinatumia misingi ya mahusiano na ukaribu kurekebisha madhara na kurejesha amani. Hatua za urekebishaji zinaweza kutumika kama hatua za uzuiaji na usaidizi. Hatua za urekebishaji zinaweza kusaidia shule kujenga mahusiano na kuwawezesha wanajamii kuwajibika kwa ustawi wao au wa wengine, kuzuia au kukabiliana na mgogoro kabla haujazidi, kujenga ukakamavu, kushughulikia sababu za msingi zinazowaongoza vijana kushiriki katika tabia isiyofaa, kukuza ujuzi wa wale ambao wamewadhuru wengine ili tabia hiyo isijirudie na kuwapa wakosaji fursa ya kuwajibika kwa waliowadhuru na kuwawezesha kurekebisha madhara hayo kadri iwezekanavyo. Zikitumika kama hatua ya usaidizi, kuchukua hatua ya urekebishaji kuadhibu hubadilisha maswali ya msingi yanayoulizwa wakati tukio la tabia isiyofaa linatokea. Badala ya kuuliza ni nani wa kulaumiwa na jinsi walioshiriki katika tabia isiyofaa watakavyoadhibiwa, hatua ya urekebishaji huuliza maswali muhimu yafuatayo:

-Nini kilichofanyika?
-Ulikuwa unafikiria nini wakati huo?
-Umefikiria kuhusu nini tangu wakati huo?
-Nani aliyeathiriwa na ulichofanya? Kwa njia gani?
-Unafikiri ni nini unachohitaji kufanya ili kurekebisha mambo? -

**‘Mali ya shule’** inamaanisha ndani au katika jengo, kiunzi, uwanja wa michezo, uwanja, sehemu ya maegesho au ardhi iliyo ndani ya mpaka wa shule ya msingi au ya sekondari ya serikali, au ndani au kwenye basi la shule, kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Magari na Trafiki (Vehicle and Traffic Law) Kifungu cha §142.

**‘Shughuli ya shule’** inamaanisha tukio au shughuli yoyote ya shule ya nje ya elimu ya darasani.

**‘Jinsia’** inamaanisha maumbile ya nje, ya kibiolojia, ya kikromosomu, ya kijenetiki na kianatomia ya mwili

**“Mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi”** inamaanisha kuvutiwa kimapenzi na watu wa jinsia tofauti na yako, jinsia moja na yako au jinsia zote mbili. Mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi wa mtu ni tofauti na utambulisho wake wa kijinsia.

**‘Mwanafunzi mwenye vurugu’** inamaanisha mwanafunzi mwenye umri wa chini ya miaka 21 ambaye:

1. Anamtendea mfanyakazi wa shule kitendo cha vurugu.
2. Anatenda kitendo cha vurugu akiwa shuleni au katika shughuli ya shule kwa mwanafunzi mwingine au mtu mwingine yeyote shuleni au katika shughuli ya shule.
3. Anapatikana na silaha akiwa shuleni au katika shughuli ya shule
4. Anaonyesha kitu kinachoonekana kuwa silaha akiwa shuleni au katika shughuli ya shule.
5. Anatishia kutumia silaha akiwa shuleni au katika shughuli ya shule.
6. Anaharibu kimakusudi na kwa kujua mali binafsi ya mfanyakazi yeyote wa shule au mtu yeyote aliye shuleni au katika shughuli ya shule kisheria.
7. Anaharibu mali ya wilaya kimakusudi na kwa kujua.

**‘Silaha”** ina maana sawa na neno “silaha hatari” kulingana na Kifungu cha 18 cha USC §930(g)(2) ambayo inajumuisha silaha, kifaa, chombo au kitu, chenye uhai au kisicho hai kinachotumika au kinachoweza kusababisha kifo au jeraha kubwa la mwili. ‘Silaha’ inamaanisha bunduki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 18 cha USC §921 kwa makusudi ya Sheria ya Kukataza Bunduki Shuleni (Gun-Free Schools Act). Inamaanisha pia bunduki nyingine yoyote, bunduki ya BB, bastola, revolva, bunduki fupi, bunduki ndefu, bunduki ya mashine, mfano wa bunduki, daga, daga fupi, wembe, kisu chembamba kirefu, kisu cha kubadilisha makali, kisu cha kuchomoka, konzi za chuma, kombeo, kisu cha konzi ya chuma, upanga wa fimbo, bunduki ya kielektroniki ya kupooza mtu, nyota ya Kung Fu, bunduki ya kielektroniki ya kuduwaza mtu, kifaa cha kupuliza pilipili au kifaa kingine cha kupuliza kitu cha kudhuru, bomu ya kulipuka au ya moto, au kifaa, chombo au kitu kingine kinachoweza kusababisha jeraha la mwili au kifo kinapotumika kusababisha jeraha la mwili au kifo.

Ingawa haijawekwa chini ya ufafanuzi wa silaha, utumiaji au umiliki wa nyembe zozote, vifaa vya kukatia baoksi, visu vya ukubwa wowote au kifaa kingine chochote kilicho na makali ya aina yoyote hairuhusiwi pia, isipokuwa iruhusiwe moja kwa moja na msimamizi. Ukipatikana na vitu vyovyote ikiwa ni pamoja na, lakini si tu vitu hivi

unaweza kuchukuliwa hatua ya adhabu.

# Kiambatisho cha B: Fomu ya Mwanafunzi ya Kuwasilisha Malalamiko ya Uchokozi na Kusumbuliwa

Kusudi la fomu hii ni kufahamisha wilaya kuhusu tukio au mfululizo wa matukio ya uchokozi au usumbufu, ili tuweze kufanya uchunguzi na kuchukua hatua zinazofaa.

Wilaya inakataza kuchokozwa na kusumbuliwa kwa wanafunzi kwa msingi wa asili ya kweli au inayodhaniwa, rangi, uzito, taifa la asili, kabila, dini, desturi za kidini, ulemavu, jinsia, mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi na utambulisho au mwonekano wa kijinsia ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu hali na mitindo ya nywele ya kujilinda ikiwa ni pamoja na, lakini si tu misuko, misokoto na mikunjo.

Ikiwa mwanafunzi anahofia usalama wake shuleni, jaza fomu hii, na tunakusihi uzungumze moja kwa moja na Mwalimu Mkuu wa Shule au Naibu Mwalimu Mkuu/Msimamizi wa DASA au Wawakilishi wake haraka iwezekanavyo ili tuweze kushughulikia wasiwasi wako.

Jina la Mwanafunzi: ____________________________________ Kitambulisho cha Mwanafunzi: ___ Gredi: ___________

Shule: ______________________________________________ Maelezo ya mawasiliano: ________________________________

1. Andika jina/majina ya mtu/watu wanaoshtakiwa kwa sababu ya uchokozi na/au usumbufu (tumia karatasi za ziada ikiwa inahitajika). _________________

______________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________________________

2. Eleza tukio/matukio. Tafadhali jumuisha wakati na mahali yalipotokea. Tafadhali tumia karatasi za ziada ikiwa inahitajika na uambatishe hati au ushahidi wowote unaohusika. ____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________

3. Ninaamini usumbufu huo unatokana na (chagua yote yanayohusika):

__ asili __ kabila __ jinsia __ rangi __ dini
__ mwelekeo wa kuvutiwa kimapenzi __ uzito __ desturi za kidini __ utambulisho au mwonekano wa kijinsia
__ taifa la asili __ ulemavu

Asili (ikijumuisha sifa zinazohusishwa kihistoria na asili hiyo, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu hali na mitindo ya nywele ya kujilinda , ikiwa ni pamoja na, lakini si tu misuko, misokoto na mikunjo),

4. Usumbufu huo unaendelea? __ Ndiyo __ Hapana

5. Tafadhali andika jina (ikiwa linajulikana) la mtu yeyote aliyeshuhudia tukio hilo au anayeweza kuwa na habari zinazohusiana na malalamiko yako. ________

______________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________________________

Swali lifuatalo si lazima lijibiwe, lakini linaweza kusaidia katika uchunguzi wa wilaya.

6. Umewahi kulalamika kuhusu au kutoa habari (kwa matamshi au maandishi) kuhusu tukio la uchokozi, usumbufu au ubaguzi au matukio kama hayo kwa wilaya? __ Ndiyo __ Hapana

Ikiwa ndiyo, lini na ulimlalamikia au kutoa habari zako kwa nani?

7. Ikiwa una wakili na ungependa tushirikiane naye, tafadhali toa maelezo yake ya mawasiliano. ______________________________________

______________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________________________

Ninathibitisha kuwa taarifa zote zilizo kwenye fomu hii ni sahihi na za kweli kadri ya ufahamu wangu.

Jina _______________________________________________ Uhusiano na mwanafunzi ____________

Saini ______________________________________________ Tarehe___________

Njia ya mawasiliano unayopendelea (tafadhali chora mviringo kwa moja): simu, barua pepe, barua, ana kwa ana
Tafadhali ambatisha hati zozote za kuthibitisha (yaani., nakala za barua pepe, madokezo, picha nk.).
Rudisha fomu hii kwa: Mwalimu Mkuu wa Shule au Naibu Mwalimu Mkuu/Msimamizi wa DASA au Mwakilishi wake.

*Dokezo la usiri:*
Ili kuchunguza malalamiko, wilaya itafichua tu yaliyomo kwenye malalamiko kwa watu walio na haja ya kujua. Fomu hii haitaonyeshwa kwa

mwanafunzi/wanafunzi/wafanyakazi walioshtakiwa.